USAID
KUTOKA KWA WATU WA MAREKANI

TZ21
21ST CENTURY BASIC EDUCATION PROGRAM

# Ufundishaji wa Kusoma

# MUONGOZO WA MWEZESHAJI WA MAFUNZO

## Toleo la Kiswahili
## Darasa la 1-2

21st Century Basic Education Program (TZ21)

## UFUNDISHAJI WA KUSOMA

# MUONGOZO WA MWEZESHAJI WA MAFUNZO

### Toleo la Kiswahili

### Darasa la I - II

**21st Century Basic Education Program**

**2013**

*Muongozo huu wa mwezeshaji wa mafunzo umechapishwa na TZ21 kwa msaada wa watu wa Marekani kupitia shirika la msaada la Marekani (USAID) na kuwezeshwa na Creative Associates International. Yaliyomo katika muongozo huu yanatokana na mwandishi na mchapishaji wake na hayawakilishi maoni na msimamo wa USAID wala Serikali ya Marekani.*

# Yaliyomo

Vifupisho ........ iv
Maelezo Muhimu kwa Mwezeshaji ........ vii
Utangulizi ........ viii
Usuli ........ ix

SIKU YA KWANZA ........ 1
Utangulizi wa kitini, Agenda na Malengo ya kujifunza ........1
Ajenda za mafunzo........ 1
Madhumuni ya Mafunzo ........ 2
Malengo mahsusi ya mafunzo ........ 2
Ufundishaji na ujifunzaji ........ 5
Majumuisho ya somo ........ 8
Mazoezi zaidi ya Ufundishaji Mzuri (saa1) ........ 15
Hitimisho ........ 19

SIKU YA PILI ........ 25
Maelezo ya jumla kuhusu vipengele vitano muhimu
katika kusoma (dk 30) ........ 27
Vipengele vitano muhimu katika ufundishaji wa kusoma ........ 28

SIKU YA TATU ........ 36
Mapitio ya mawasilisho ya siku iliyotangulia (dk 30)........ 36
Maelezo ya jumla kuhusu mpango wa kusoma ........ 40
Kufahamu muongozo wa mwalimu ........ 45

# Vifupisho

| | |
|---|---|
| **TZ21** | 21st Century Basic Education Program |
| **IYF** | International Youth Foundation |
| **USAID** | United States Agency for International Development |
| **Dkt** | Daktari |
| **TEHAMA** | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| **WEMA** | Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali |

# Shukurani

Mpango wa  Elimu wa TZ21 unapenda kutoa shukrani za dhati kwa watu wote  kwa kutoa msaada wa kiufundi, kitaaluma na kifedha ambao umesaidia katika maendeleo, tafsiri, kuhariri na kuchapisha hiki kitini cha kumfundishia mwalimu. Shukurani za pekee zinaelekezwa kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Zanzibar, Taasisi ya Elimu Tanzania, Vyuo vya Ualimu, Dkt Diane Prouty na Lynn Evans (wataalamu wa usomaji kutoka ofisi ya Creative Washington ), Msimamizi Mkuu wa Programu (Renuka Pillay) kwa ajili ya mpango wa Elimu na walimu wa skuli za Msingi.

Katika hali halisi si rahisi kuutaja kila mchango uliotolewa kufanikisha kazi hii. Waalimu wengi wenye moyo wa kujitolea na wataalamu mbalimbali walishiriki katika kazi hii.Tunapenda kuwataja baadhi yao.

| | |
|---|---|
| **Maryam Abdullah Yusuf** | Kamishna wa Elimu kutoka WEMA Zanzibar |
| **Yahya I.  A'wakr** | Mkaguzi Mkuu wa Elimu kutoka WEMA Zanzibar |
| **Sichana H. Foum** | Mkurugenzi  wa Shirika la Huduma za Maktaba  kutoka WEMA Zanzibar |
| **Uleid Juma Weldi** | Mkurugenzi wa Elimu ya Maandalizi na Msingi kutoka WEMA Zanzibar. |
| **Ameir S. H. Njeketu** | Mkurugenzi wa Baraza la Mitihani kutoka WEMA Zanzibar |
| **Suleiman Y. Ame** | Mkurugenzi wa Taasisi ya Elimu kutoka WEMA  Zanzibar |
| **Omar Said Ali** | Mkurugenzi wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kutoka  WEMA Zanzibar |
| **Charles Nonga** | Msimamizi Msaidizi wa Programu TZ21 Zanzibar. |
| **Mohamed Ali Mohamed** | Mkuza Mitaala Mkuu wa Taasisi ya Elimu  kutoka WEMA Zanzibar. |
| **Said S. Al – Abry** | Mkuu wa Divisheni wa Kituo cha Taifa cha Walimu (NTRC) kutoka WEMA Zanzibar. |
| **Ame J. Khatib** | Afisa wa Elimu ya Msingi kutoka WEMA Zanzibar. |
| **Hassan Khamis Juma** | Mkuu wa Utayarishaji wa Vitabu kutoka Maktaba Kuu Zanzibar. |
| **Hamad P. Simai** | Mkuu wa Divisheni ya Usanifu wa Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia |
| **Othman Sharif** | Mtaalamu wa Utafiti na Kumbukumbu kutoka TZ 21 Zanzibar. |

| | |
|---|---|
| **Lawrence Kunambi** | Mratibu wa Mitaala kutoka Taasisi ya Elimu Tanzania |
| **Brandina Milumba** | Mkaguzi wa Skuli kutoka Manispaa ya Mtwara |
| **Zahor Mwalim Muhidin** | Mkufunzi kutoka Chuo cha Kiislamu |
| **Ali Mwalim Rashid** | Mtaalamu wa lugha kutoka Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar |
| **Hamisi Mwaya** | Mkufunzi Chuo cha Ualimu Kitangili |
| **Zainabu Ngwende** | Mwalimu kutoka Skuli ya Msingi Mbawara - Mtwara |
| **Maulid Lipagati** | Mwalimu kutoka Skuli ya Msingi Mambeleketele - Mtwara |
| **Veronica Macha** | Mwalimu kutoka Skuli ya Msingi Chang'ombe Dar es Salaam |
| **Mary Simumba** | Mwalimu kutoka Skuli ya Msingi Mbuyuni Dar es Salaam |
| **Royce Nyoni** | Mwalimu kutoka Skuli ya Msingi Mbuyuni Dar es Salaam. |
| **Subira Idd Hamisi** | Mwalimu kutoka Skuli ya Msingi Mkunazini Zanzibar |
| **Fatuma Karande** | Mwalimu kutoka Skuli ya Msingi Kibasila Mtwara |
| **Aristarick Lyimo** | Mratibu wa Mradi kutoka Mradi wa Vitabu vya Watoto |
| **Justin Machela** | Mtaalamu wa Elimu ya Msingi kutoka TZ21 Mtwara. |
| **Joseph Mbasha** | Mratibu wa Mafunzo kutoka ofisi za TZ21Dar es Salaam. |
| **Asha M Ahmed** | Mtalaamu wa Elimu kutoka TZ21 Zanzibar |
| **Mashauri Heriel** | Afisa Manunuzi na TEHAMA kutoka TZ21 Dar es Salaam. |
| **Daud Kweba** | Afisa Usimamizi na Tathmini kutoka TZ21 Dar es Salaam. |
| **Douglas Bell** | Mkurugenzi kutoka IYF |
| **Hassan Libingai** | Mratibu Msaidizi wa Mradi wa Vitabu vya Watoto kutoka Zanzibar. |
| **Dkt Rest Lasway** | Mshauri wa Sera kutoka TZ21 Dar es Salaam. |
| **Andrew Muya** | Mratibu Msaidizi wa Mradi kutoka Mradi wa vitabu vya watoto - Mtwara. |
| **Cresencia Ngasoma** | Mwalimu kutoka Skuli ya Msingi Maktaba - Ilala Dar es Salaam. |
| **Saada S Rashid** | Mratibu Kituo cha Waalimu Bububu Zanzibar |
| **Adrehem Kayombo** | Mtalaam wa Mitaala ya Elimu kutoka TZ21/IYF Dar es Salaam. |
| **Vincent Katabalo** | Meneja wa Mafunzo ya Waalimu kutoka TZ 21 Dar es Salaam. |

# Maelezo Muhimu kwa Mwezeshaji

Muongozo huu ni kwa mwezeshaji atakayeshiriki mafunzo yanayowalenga walimu wanaofundisha Kiswahili darasa la kwanza na la pili. Muongozo huu utatumika sanjari na kitini cha mafunzo ya walimu, muongozo wa mwalimu katika ufundishaji wa usomaji na mawanda na mtiririko wa kufundisha usomaji kwa darasa la kwanza. Hali kadharika, muongozo huu utamsaidia mwenzeshaji kuwa na mpangilio mzuri wenye kufuata hatua kwa hatua ili kumfanya mshiriki wa mafunzo kushiriki kikamilifu katika kujifunza njia fanisi za ufundishaji na ujifunzaji wa usomaji.

Maudhui yaliyo katika muongozo huu yatawasilishwa na wawezeshaji kwa muda wa siku tatu.  Ni wazi kuwa muda hautoshi kukidhi mahitaji. Kwa mantiki hii, mwezeshaji anashauriwa kutenga muda wa kutosha wa kuusoma muongozo huu kwa ufasaha ili aweze kujiamini na kumudu mada atakazoziwasilisha wakati wa mafunzo.


Alama zifuatazo zitamwongoza mwezeshaji katika kusoma na kuuelewa muongozo huu:





Alama hii itakuonesha muda utakaotumika kwa kila mada wakati wa mafunzo



Alama hii maana yake mapitio



Alama hii inakuonesha kazi za kufanya kwa mshiriki mmoja mmoja, jozi au kwa vikundi



Alama hii inaonyesha ufupisho wa mada iliyofundishwa

# Utangulizi

Mpango wa Elimu TZ21 unafadhiliwa na Shirika la Misaada la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani (USAID) na unatekelezwa na Creative Associates kwa ushirikiano na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kutoka Tanzania Bara na Zanzibar. Mpango huu unashirikiana na wizara zote mbili katika mambo mengi kama vile kuendeleza rasilimali watu katika elimu, kuimarisha mfumo wa usimamizi wa taarifa za elimu na sera ili kuimarisha kiwango cha elimu Tanzania.

Kuimarisha kiwango cha wanafunzi wanaojua kusoma katika madarasa ya awali ya shule za msingi ni moja ya malengo makuu ya Mpango wa Elimu TZ21. Kupitia TZ21, utekelezaji wa njia za usomaji zitasaidia ufundishaji na ujifunzaji makini wa kusoma katika madarasa ya awali ya shule za msingi.

Kiutekelezaji, mpango huu unakusudia kuendesha mafunzo kwa waalimu wa shule za msingi, walimu wakuu wa shule, Waratibu wa Elimu Kata, Waratibu wa Vituo vya Elimu juu ya ufundishaji makini wa kusoma katika madarasa ya awali kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Mpango huu unasimamia vipengele vitano muhimu ambavyo wanafunzi lazima wavisome ili waweze kusoma kwa ufasaha. Vipengele vyenyewe ni kama ifuatavyo ; (1) utambuzi wa umbo sauti, (2) kanuni za kialfabeti/ fonetiki, (3) ufasaha, (4) msamiati, (5) ufahamu. Mjumuisho wa stadi hizi na ujuzi ambao umejengwa katika mazoezi yenye kuleta ufanisi ndiyo ambayo yamejenga maudhui ya mafunzo kwa walimu wa darasa la kwanza na pili.

Kitini hiki cha kumfundishia mwalimu kinatilia mkazo kwenye mazoezi bora ambayo walimu wanatumia kufundishia kusoma, mtazamo, muonekano mzima wa mtaala wa kusoma na mfumo mzima wa tathmini. Zaidi ya hayo, mazoezi hayo hayo yanayotumika katika kufundisha kusoma yanaweza pia kutumika katika kufundisha mada yoyote katika masomo mengine.

Mifano iliyotumika imejumuisha stadi zote za msingi katika kusoma kama vile utambuzi wa umbosauti, utambuzi wa wa herufi na sauti ya herufi. Ingawa kitini hiki cha kufundishia kinatilia mkazo kwenye Kiswahili, njia zitumikazo ni sahihi na zinafaa kufundishia lugha yoyote ile, kikiwamo Kingereza.

# Usuli

Tunawezaje kuwafundisha wanafunzi kusoma kwa ufasaha, kwa haraka, na ufahamu katika madarasa ya awali? Tafiti za kisayansi zilizolenga usomaji zinaelekeza maeneo makuu matano muhimu katika kumfanya mtoto awe msomaji hodari. Maeneo hayo ni:

- Utambuzi wa umbo sauti ***(fonolojia)*** yaani uwezo wa kusikia, kutambua na kuitawala sauti mojamoja;
- Uhusiano wa sauti na herufi (***Fonetiki)*** yaani kutambua uhusiano uliopo kati ya sauti na herufi ili kuunda silabi na maneno
- Kusoma kwa ufasaha
- Msamiati
- Ufahamu.

***Ufundishaji unaozingatia maelekezo ya wazi hatua kwa hatua***

- Maelekezo yanatakiwa yawe yamepangwa, yenye malengo, na yanayoeleweka.
- Yafuate mtiririko wenye mantiki ulioratibiwa
- Ufundishaji ushabihiane na maudhui katika somo
- Msisitizo ulenge kukidhi mahitaji ya kujifunza ya mwanafunzi mmoja mmoja au kikundi
- Kuwe na ufuatiliaji wa taarifa za maendeleo ya usomaji ya mwanafunzi kwa kila hatua.

Katika muktadha huu, pia tafiti zinaonesha kuwapo kwa mitazamo tofauti katika kufundisha usomaji kwa kutumia vipengele vitano vilivyotajwa hapo juu.

Tofauti hizo zinajitokeza katika namna walimu wanavyotoa muongozo na maelekezo kwa wanafunzi katika kujifunza maarifa mapya. Tofauti nyingine hutegemea walimu wanavyoonesha kwa vitendo namna sahihi ya kutumia maarifa mapya. Hali kadhalika, tofauti nyingine zinazojitokeza ni namna mwalimu anavyozingatia mtiririko wenye mantiki katika kufundisha maarifa mapya.

Muongozo huu umeundwa na vipengele vitano vinavyomsaidia mwalimu katika kufundisha usomaji na uandikaji. Vipengele hivyo ni:

- Utambuzi wa umbosauti (Fonolojia)
- Uhusiano wa maumbo sauti na herufi (Fonetiki)
- Msamiati
- Kusoma kwa ufasaha
- Ufahamu

Kila kipengele katika muongozo huu kina utangulizi na muundo wa kufundisha maudhui yaliyokusudiwa. Muundo huu pia, umewekwa katika chati inayoonesha kazi ya mwalimu, mwalimu na mwanafunzi na mwanafunzi pekee kama ifuatavyo:

# Ratiba ya Mafunzo

## Siku ya kwanza

| Muda | Shughuli |
|---|---|
| 2:30 – 3:00 | Usajiri, Ukaribisho na Utambulisho (dakika 30) |
| 3:00 – 04:00 | Maelezo ya juml ya mazoezi ya ufundishaji makini |
| 04:00 – 04:30 | Mapumziko |
| 04:30 – 05:30 | Maelekezo Mzunguko Sehemu ya 1( saa 1 ) |
| 05:30 – 06:30 | Mzunguko wa Somo ( saa 1 ) |
| 06:30 – 07:00 | Majadiliano katika Vikundi ( dakika 30) |
| 07:00 – 08:00 | Chakula cha Mchana (saa 1 ) |
| 08:00 – 08:30 | Zaidi kuhusu Mazoezi Mazuri (dakika 30 ) |
| 08:30 – 10:00 | Majumuisho ( saa 1 na dakika 30) |

## Siku ya pili

| Muda | Shughuli |
|---|---|
| 02:30 – 03:00 | Kupitia kwa Ufupi Vipengele Muhimu vya Maudhui ya Siku ya Kwanza (dakika 30 ) |
| 03:00 – 03:30 | Utangulizi wa Maelekezo ya Usomaji (dakika 30 ) |
| 03: 30 – 04:00 | Maelezo ya Jumla ya Vipengele 5 Muhimu vya Usomaji (dakika 30 ) |
| 04:00 – 04:30 | Mapumziko (dakika 30 ) |
| 04:30 – 06:00 | Mwamko wa Mfumo wa Sauti (saa 1 ) |
| 06:00 – 07:00 | Ufundishaji wa Utambuzi wa Sauti Zinazowasilishwa na Herufi/ kanuni za kialphabeti (saa 1 ) |
| 07:30 – 07:00 | Majadiliano katika Vikundi (dakika 30) |
| 07:00 – 08:00 | Chakula cha mchana (saa 1 ) |
| 08:00 – 09:00 | Ufasaha wa Lugha (saaa 1 ) |
| 09:00 – 10:00 | Majadiliano katika Vikundi ( saa 1 ) |

## Siku ya tatu

| Muda | Shughulia |
|---|---|
| 02:30 – 03:00 | Kupitia kwa Ufupi Vipengele Muhimu vya Maudhui ya Siku ya Pili (30 minutes) |
| 03:00 – 04:00 | Msamiati (saa1 ) |
| 04:00 – 04:30 | Mapumziko (dakika 30 ) |
| 04:30 – 06:30 | Maelezo ya Jumla kuhusu Mtaala wa Usomaji. (saa 2 ) |
| 06:30 – 07:00 | Majadiliano katika vikundi (dakika 30) |
| 07:00 – 08:00 | Chakula cha Mchana (saa 1 ) |
| 08:00 – 09:00 | Tathmini(saa 1) |
| 09:00 – 10:00 | Majumuisho ( saa 1 ) |

## SIKU YA KWANZA

### Ukaribisho na utangulizi (dk 30)

Waongoze washiriki wa mafunzo kuweka taratibu zitakazoongoza mafunzo. Taratatibu zinaweza kuwa kama zifuatazo kuweka simu kwenye mtetemo; na zile ambazo hazina teknolojia hiyo zizimwe, kujali muda, kuheshimu mawazo ya kila mshiriki na kushiriki kikamilifu katika mafunzo.

Tunaanza mafunzo ya leo kwa wimbo:

*Asiyependa Shule ni mjinga kabisa*
*Asiyependa Shule ni mjinga kabisa*
*Barua ikija aitembeza kutwa*
*Barua ikija aitembeza kutwa.*

**Utangulizi wa kitini, Agenda na Malengo ya kujifunza**
**Mapitio ya kitini cha mwalimu**

Ndugu mwezeshaji, hakikisha kuwa kila mshiriki wa mafunzo ana kitini cha kujifunzia chenye kuwa na mambo yote yanayohitajika katika mafunzo kama vile muongozo wa ufundishaji kusoma kwa darasa la kwanza au la pili, kitini cha mafunzo na mawanda na mtiririko wa kufundisha usomaji kwa darasa la kwanza au la pili.

**Mapitio ya Ajenda**

Ndugu mwezeshaji waongoze washiriki kufungua kitini kwenye ukurasa wa 8-9 unaoonesha mambo utakayojifunza kwenye mafunzo haya. Katika kipindi cha siku 3 zijazo, mafunzo yatatilia mkazo mazoezi ya ufundishaji unaoweza kutumika kufundishia mada yoyote ile. Mafunzo haya yanakusudia kukuza taaluma ya ufundishaji mzuri, vitu vitano muhimu katika kufundisha kusoma na maelezo ya jumla ya mpango wa kusoma na tathmini ambavyo ni msingi ufundishaji bora wa kusoma.

### Ajenda za mafunzo ni kama ifuatavyo

**Siku ya Kwanza**

- Maelezo ya jumla na kubadilishana uzoevu kuhusu ufundishaji mzuri (dk 30)
- Mfumo wa ufundishaji (saa 1)
- Mfumo wa somo (saa 1)
- Mifano miwili zaidi ya ufundishaji mzuri (saa 1)
- Majumuisho (masaa 2)

**Siku ya pili**

- Utangulizi kuhusu kujifunza usomaji (dk 15)
- Umuhimu wa kujifunza kusoma mapema (dk 15)
- Maelezo ya jumla kuhusu vipengele 5 kuhusu kusoma (dk 30)
- Uelewa wa umbo sauti (saa 1.30)
- Fonetiki (saa 1.30)
- Kusoma kwa kasi (saa 1.30)

**Siku ya tatu**

- Msamiati (saa 1)
- Ufahamu (saa 1)
- Maelezo ya jumla kuhusu mpango wa kusoma (saa 1)
- Muongozo wa mwalimu na daftari la mwanafunzi la kufanyia kazi (saa 1)
- Tathmini (saa 1)

## Madhumuni ya Mafunzo



***Mapitio ya mafunzo na malengo ya ujifunzaji***
***Baada ya Mafunzo haya ya siku 3, washiriki wote wa mafunzo haya (walimu)watakuwa na uwezo wa:***

- Kupata ujuzi wa kufundisha kwa ufasaha.
- Kuhusianisha maudhui na mafunzo.
- Kutumia njia bora za ufundishaji.
- Kufanya mazoezi ya kila siku kuhusu mpango wa usomaji.
- Kuendesha masomo kwa kutumia mbinu mpya.

## Malengo mahsusi ya mafunzo ni kama ifuatavyo

**Ufahamu: utoaji wa maarifa**

- Walimu (washiriki) wanakuwa na uwezo wa kuelezea ufundishaji bainifu, ulio katika mpangilio mzuri wenye kuzingatia mpango wa usomaji.
- Walimu waweze kubaini vipengele vya muongozo wa mwalimu.
- Walimu waweze kubaini matumizi sahihi ya mifumo mbalimbali ya kupanga makundi.


**Ufahamu: Maudhui na taaluma ya ufundishaji**.

Washiriki wawe na uwezo wa kuelezea na kuonesha mahusiano yaliyopo baina ya maudhui na taaluma ya ufundishaji.

**Matumizi: Uandaaji wa somo**
Walimu wawe na uwezo wa kuandaa somo kwa kutumia mbinu mpya.

**Matumizi : Utaratibu wa kila siku wa mpango wa usomaji**
Walimu wawe na uwezo wa kueleza na kuonesha kwa vitendo namna ya kuhusianisha na kuzipanga kwa usahihi kazi zote kwenye mpango wa usomaji.

## Maelezo ya jumla kuhusu njia bora za kufundishia na kujifunzia (dk 30)



**Kazi ya kufanya katika vikundi: Mapitio ya ufundishaji mzuri**
**Maelekezo**
Waambie washiriki wapitie mazoezi yaliyo hapa chini wakiwa katika vikundi vya watu watano mpaka kumi. Onesha jinsi dhana hizi zinavyohusiana na ufundishaji mzuri na maana zake. Kumbuka ya kuwa taarifa hii ilifanyiwa kazi kwenye mafunzo yaliyopita.
Ndugu mshiriki una dakika 5 za kufanya kazi hii.

- Kuandaa somo
- Utangulizi wa somo
- Matumizi ya vifaa vya kufundishia
- Mazoezi na mrejesho
- Mazoezi endelezi
- Kujifunza kwa vitendo
- Kuendeleza kujifunza

### Ufafanuzi

| | |
|---|---|
| 4 | Mwalimu anatoa fursa kwa wanafunzi kupokea mrejesho kwa kadiri wanavyofanya mazoezi ya ujuzi wajifunzao.. |
| 5 | Mwalimu anatumia njia mbalimbali kuona kama wanafunzi wamejifunza somo lolote ama la. |
| 3 | Mwalimu anatumia nyenzo mbalimbali kusaidia ufundishaji wa somo. |
| 1 | Mwalimu amejiandaa kwa somo na ana fahamu fika matokeo yake, shughuli zinazofaa kwa somo, vifaa vya lazima vya kufundishia na nyenzo za tathminia. |
| 6 | Mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wanashirikishwa katika kazi ya kujifunza. |
| 7 | Mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wana shughuli sahihi kwa kufanyia mazoezi maarifa mapya nje ya shule. |
| 2 | Mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wako tayari kujifunza kwa kuwaambia kwa lugha rahisi wanacho tarajia kujifunza. |

**Kubadili uzoefu  wa mwanafunzi**

Wakumbushe washirki kuwa  ufundishaji na ujifunzanji ni pande mbili za sarafu moja, na huwa kuna ulazima wakujali nini kimefundishwa na kiwango cha uelewa cha mwanafunzi.Wote walimu na wanafunzi wana wajibu wa kushiriki katika kutoa na kupokea stadi wakati  wa ufundishaji na ujifunzaji.
Sisi kama walimu,tuna wajibu wa kubadili uelewa wa wanafunzi kama hawajifunzi kitu chochote.


Kuna namna tatu za kubadili uelewa wa mwanafunzi

- Kiwango cha ufundishaji ambacho mwanafunzi anakipata
- Mkazo unaotiliwa katika ufundishaji na ujifunzaji.
- Ubora wa ufundishaji na ujifunzaji.

Tunaweza kuongeza kiwango cha kujifunza anachopokea mwanafunzi kwa kuwa na ufundishaji wenye mpangilio, kuzingatia matumizi bora ya muda, na mazoezi ambayo yanamshirikisha mwanafunzi kikamilifu.

Tunapobainisha na kupanga vipaumbele vya stadi na ujuzi kuwa ndiyo lengo la ufundishaji  kwa kumshirikisha mwanafunzi, tunakuwa tumeongeza kiwango cha mwanafunzi cha kujifunza.mazoezi.

Mwisho tunaimarisha  ufundishaji na ujifunzaji pale tunapotumia vitendo vya ufundishaji mzuri, tutumie taarifa za uelewa wa mwanafunzi kupanga na kuboresha na hivyo kujitathmini sisi walimu juu ya namna tunavyofanya kazi yetu.



**Tafakuri (dk 5)**
**Kazi ya kufanya kwa mshiriki binafsi: Marudio**

**Kazi za ufundishaji na ujifunzaji**

Waagize kila mshiriki  kuandika muda anaoutumia katika  ufundishaji na ujifunzaji. Hii ni kazi binafsi hampaswi kushirikiana. Hii itawawezesha ninyi kuwa makini juu ya matumizi ya muda. Utatakiwa kutumia mada hii kadri tunavyoendelea na mafunzo.

Kupanga ________________
Kuandaa vifaa vya kufundishia na kujifunzia_________________
Kufundisha_________________
Kurekebisha tabia na mwenendo wa wanafunzi___________________
Kusahihisha na kutunza kumbukumbu za kazi za wanafunzi_______________

## Ufundishaji na ujifunzaji

### kuelewa jinsi wanafunzi wanavyojifunza

Wakumbushe washiriki kuwa ili kujua namna ya kufundisha vizuri, yatupasa kuelewa namna gani wanafunzi wanajifunza mambo mbalimbali. Kujifunza ni mazoezi ya kila siku katika maisha. Karibu kila kitu tunachojifunza, tunajifunza kwa wakati husika.

Katika mazingira ya darasani tunaweza kutazama tendo la kujifunza katika mitizamo miwili:

- **Mzunguko katika ufundishaji na ujifunzaji**
  unaelezea juu ya aina ya mafunzo yanayohitajika kwa muda muafaka.
- **Mzunguko wa somo**
  unaelezea utaratibu unaotumika kwa kila somo

**Mzunguko katika ufundishaji na ujifunzaji (saa 1)**

Ufundishaji na ujifunzaji una mambo matatu ambayo hutolewa kulingana na muda

- Utangulinzi wa stadi mpya au mbinu
- mazoezi
- Majumuisho

**Stadi:** Tambua na taja herufi inayokusudiwa**.**
**Malengo ya ufundishaji na ujifunzaji:** Herufi inayokusudiwa imeoneshwa, mwanafunzi ataitaja herufi hiyo.
**Maandalizi ya awali:** Toa utangulizi wa kile ambacho wanafunzi watakuwa wakikifanya na kwanini ni muhimu kujifunza.
**Mwalimu "**Leo,tutajifunza herufi mpya. Nitawaonesha herufi, na kisha nitakueleza jina la herufi **m"**
**Kazi mfano:** Onesha herufi inayokusudiwa, elekeza kwenye herufi inayokusudiwa wambie kuwa**:**
**Mwalimu**: "Herufi hii ni___**m**___**"**
**Mazoezi elekezi:** Onesha herufi inayokusudiwa, elekeza kwenye herufi inayokusudiwa na sema yafuatayo:
**Mwalimu : "**Tuseme wote kwa pamoja. Herufi hii ni m"
**Mwalimu na mwanafunzi:** Tuseme jina la herufi kwa pamoja
**Mazoezi binafsi:** Waruhusu wanafunzi wafanye mazoezi wao wenyewe kwa kujitegemea.
**Mwalimu: "**Sasa unaweza kujaribu. Herufi hii inaitwa **m"**
**Wanafunzi:** Taja jina la herufi**.**
**Kukazia Maarifa:** Onesha herufi inayokusudiwa na kisha wanafunzi wataje jina la herufi, kisha waeleze wanafunzi waandike herufi inayokusudiwa.

- **Utangulizi wa stadi mpya au mbinu**

Ufuatao ni mfano wa utangulizi wa somo ambalo lengo lake ni kufundisha stadi mpya

***Utangulizi wa somo***

Ndugu mwezeshaji waambie washiriki kuwa, dondoo zifuatazo hapo chini zinaonesha vipengele sita vya somo : stadi, malengo ya ufundishaji na ujifunzaji, maandalizi awali, mazoezi elekezi, mazoezi binafsi na tathmini.

- **Stadi ndiyo lengo katika ufundishaji na ujifunzaji.**

  Lengo la ufundishaji na ujifunzaji linaonesha mwanafunzi atajifunza nini na jinsi watakavyoonesha kitu au vitu ambavyo wamejifunza.

  **Maandalizi awali** : Wanafunzi waelezwe kitu wanachotakiwa kujifunza. Hii itavuta usikivu wao kwa kugundua kwanini ni muhimu kujifunza mada husika.

  **Kazi mfano**: Hatua hii inawapa wanafunzi mfano unaoonesha namna watakavyofanya kazi na jinsi ya kutumia mbinu fanisi wakati wa kujifunza.

  **Mazoezi elekezi :** mazoezi haya yanawasaidia wanafunzi kufanyia mazoezi stadi mpya au mbinu mpya kwa kupata msaada kutoka kwa mwalimu wakati wanapoweza kukamilisha kazi kwa usahihi,watafaanya mazoezi wao wenyewe kwa kujitegemea.

- **Kulifanyia mazoezi somo:**

  Hatua ya pili katika mzunguko wa ufundishaji na ujifunzaji ni kufanya mazoezi. Baada ya kuitambulisha stadi mpya au mbinu. Wanafunzi watatakiwa kufanyia mazoezi na walimu wao,wakiwa kwenye vikundi au mmoja mmoja kwa kujitegemea.

***Tuangalie mazoezi katika somo lifuatalo linatuonesha mazoezi yanayohusu stadi iliyotolewa.***

## Kufanya mazoezi ya somo

**Stadi:** Tambua na taja herufi inayokusudiwa.
**Malengo ya ufundishaji na ujifunzaji**: herufi inayokusudiwa inaoneshwa, mwanafunzi atataja herufi husika.

**Maandalizi awali:** tambulisha kitu kile ambacho mwanafunzi anatarajia kujifunza na kwa nini ni muhimu kwake kujifunza'

**Mwalimu: "**Leo tutafanya mazoezi kutamka herufi ambazo tumejifunza. kwanza tutazirudia kisha tutazifanyia mazoezi

**Marudio:** Onesha herufi zote ambazo wanafunzi wamejifunza wiki hii na kisha watajie jina lake.

**Kazi mfano: O**nesha kazi ya kufanyia mazoezi
**Mwalimu**: "Leo tutacheza mchezo. Nitakuonesha herufi nanyi mtaitamka kwa sauti kubwa kisha mtatafakari juu ya herufi M na utasema kama jina lako linaanzia na herufi M. Nitahesabu mara tatu na ikiwa herufi M ipo katka jina lako utasimama."

**Mazoezi elekezi**: Onesha kila herufi mara moja na kwa wakati mmoja.

**Mwalimu**: "Tufanye mazoezi kwa pamoja, kwanza kabisa ,tutaje jina wote kwa pamoja. Jina la heurfi hii ni M"

**Mwalimu na mwanafunzi**: Taja jina la herufi.


**Mwalimu**: Sasa fikiri kuhusu herufi. Ninahesabu mpaka tatu, na ikiwa herufi M imo katika jina lako utasimama. Nahesabu 1, 2, 3……………………..

**Wanafunzi**: Wanafunzi ambao majina yao yanaanza na herufi hiyo wanasimama juu.

**Mazoezi binafsi** : Mwanafunzi afanye mazoezi peke yake pasipokusaidiwa.

**Mwalimu:** "Jaribu kutamka herufi. Herufi hii ni M"

**Mwanafunzi:** atataja jina la herufi
**Mwalimu**: 'Fikiri, moja, mbili, tatu
**Wanafunzi:** Mwanafunzi asimame kama herufi M ipo kwenye jina lake.
**Matumizi**: Endelea na herufi zote na rudia kadri inavyotakiwa.



**Kazi ya kufanya katika jozi na vikundi: Linganisha masomo mawili - fikiri - shirikishana katika jozi**
**Kazi ya ufundishaji na ujifunzaji**

Mwezeshaji awaagize washiriki kujadiliana katika jozi. Swali la kujadiliana linauliza "ni kwa namna gani kazi za utangulizi zinatofautiana na kazi za mazoezi?"

Kwanza, fikiria jibu peke yako, kisha jadiliana na mwenzako kwenye vikundi . Baada ya dakika 2, waagize kila jozi kuwasilisha majibu yao katika vikundi

## Majumuisho ya somo

Mwezeshaji afafanue kuwa, aina nyingine ya somo ni majumuisho ya somo. Lengo la majumuisho ya masomo ni kutoa fursa kwa wanafunzi kufanyia mazoezi kitu au vitu ambavyo wamejifunza katika muktadha mpya. Hii inamaanisha kuwa tunalenga mwanafunzi atumie uelewa ambao ameupata kwa utaratibu mpya.

Sasa tuangalie katika majumuisho ya somo. Katika somo hili, tutapitia upya utaratibu na kuwapatia wanafunzi jina la herufi na kuuliza kama wanaweza kuandika au kuonesha herufi.

### Majumuisho ya somo

**Stadi:**Tambua herufi inayokusudiwa
**Malengo ya ufundishaji na ujifunzaji:** Kwa kuzingatia herufi inayokusudiwa, mwanafunzi atachagua herufi sahihi miongoni mwa herufi tano zilizotolewa**.**
**Maandalizi awali:** Anza kwa kuwambia wanafunzi kile watakachokifanya na kile ambacho watatakiwa kujifunza**.**
**Mwalimu :** "Leo tutajifunza mchezo katika kikundi chenu. Kila mmoja atakuwa na herufi tano. Kila mtu katika kikundi atatamka herufi aliyonayo na wengine wote mtaonesha herufi iliyotajwa.
**Mazoezi elekezi:** Onesha kila herufi mara moja kwa wakati mmoja
**Mwalimu**: Herufi hii ni___
**Mwalimu na wanafunzi :** Taja jina la herufi.
**Mazoezi binafsi** : Wanafunzi wote watafanya mazoezi kwa kujitegemea pasipo kusaidiwa na mwalimu.
**Mwalimu** : Sasa chezeni mchezo wa herufi kwenye vikundi vyenu
**Matumizi**: Fuatilia vikundi wakati vinapocheza mchezo wa herufi.

**Kazi ya kufanya katika jozi: Linganisha masomo kwa kutumia mbinu ya fikiri - jozisha**

**Kazi za Ufundishaji na ujifunzaji**

Mwezeshaji awasaidie washiriki kulinganisha mifano ya somo. Swali watakalojadili katika jozi ni "Ni kwa namna gani kazi za utangulizi na kazi ya mazoezi zinatofautiana na kazi za majumuisho?"

**Ufupisho**

Mwezeshaji atoe maelezo ya kina na kwa ufupi kuwa mzunguko wa ufundishaji na ujifunzaji huzingatia namna kazi ya ufundishaji na ujifunzaji inavyofanyika. Kazi za utangulizi katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi mpya au mbinu mpya husaidia kuwaendeleza wanafunzi kwa kuwajengea ujuzi. Kazi za mazoezi hutoa mazoezi au pitio za stadi ambazo wanafunzi wamejifunza.

Hata hivyo, huhitaji bado mazoezi ya ziada ili kuwawekea uelewa moja kwa moja (Automaticity). Ujengaji wa uelewa moja kwa moja ni kitendo cha kupata taarifa haraka kama vile kutambua haraka herufi, matamshi na herufi husika. Kazi za majumuisho hutoa nafasi kwa wanafunzi kutumia stadi walizonazo katika kujifunza kwenye mazingira mapya. Wakati wanafunzi wanapojumuisha uelewa wao wa stadi, wanaweza wakatumia uelewa huo hata wakiwa peke yao.

Mzunguko huu wa kazi za utangulizi, mazoezi na majumuisho huunda mfumo ambao wanafunzi hujifunza stadi mpya, huzipitia na kisha kuzitumia.


Kila mara tunapofundisha dhana tunatumia mzunguko huu katika kujenga msingi wa stadi na mbinu ambazo mwanafunzi anaweza kuzitumia wakati wa kujifunza.

**Mzunguko wa somo (saa 1)**

Mwezeshaji awafafanulie washiriki kuwa katika aina tatu za mada ambazo tumezifanyia kazi, utakuwa umejifunza kuwa kuna mfumo usiobadilika katika ufundishaji na ujifunzaji.

Kwa kutumia mfumo huu, tunaweza kuwasaidia walimu kuweka mazingira mazuri ya ujifunzaji, wakaweza kutumia vizuri muda wa kufundishia na kujifunzia na kutumia njia bora za ufundishaji. Mzunguko wa somo unatoa mpango mzuri kama inavyooneshwa kwenye kielelezo namba 1

**Kielelezo 1: Mzunguko wa somo**




## Vipengele fanisi vya somo

Kuna vipengele vitano vya somo fanisi kama linavyoonekana hapo juu.

- **Maandalizi awali**
  Maandalizi awali inawapatia mwanafunzi kitu watakachojifunza na kwa nini ni muhimu wao kujifunza.

- **Kazi mfano**
  Walimu wanatakiwa kueleza kwa uwazi , kuonesha kwa mifano na mazoezi ya kutosha kuondoa utata wakati wa utaratibu wa ufundishaji na ujifunzaji. Unapaswa kuonesha lengo kwa kutoa mifano bainifu na kufuata hatua kwa hatua wakati wa kufafanua dhana, stadi na kazi husika ili kuufanya mazoezi ya kufundisha na kujifundisha yawe fanisi.

Kuna aina mbili ya mfano elekezi ambayo walimu wanaweza kutumia:

- Kazi inayokusudiwa iwe inaeleweka wazi na wala isiwe na utata wa aina yoyote
- Utaratibu utakaotumiwa katika kukamilisha mazoezi uwe bainifu .



**Kazi ya kufanya kwa kila mshiriki: Kubaini aina ya kazi mfano Mazoezi ya ufundishaji na ujifunzaji**

Mwezeshaji anawasilisha kila kazi mfano. Utaonesha kidole kimoja kuashiria kazi, na vidole viwili kuashiria utaratibu elekezi.

Baada ya majadiliano na washiriki mwezeshaji atatoa ufafanuzi wa majadiliano kwa kuongozwa na jedwali hapa chini:

**KIDOLE KIMOJA** (ni jibu sahihi kwa mfano huu hapa juu**,** kwa sababu *ni kazi…inakuelekeza nini cha kufanya, lakini haikuelezi hatua mbalimbali katika utaratibu wa kufundisha)*

Nitawatajia neno moja kwa wakati mmoja nanyi mtaniambia ama neno hilo linaanza na sauti /m /au la. Kama neno linaanza na sauti, onesha ishara ya kidole gumba juu. Kama neno halianzi na sauti, onyesha kidole gumba chini.

T: Neno la kwanza, *meza*. Nasema mwenyewe kimya kimya, *meza.* Natofautisha sauti ya kwanza /m/. Neno *Meza* linaanza na /m/ hivyo nanyoosha kidole gumba changu juu.

T: Neno linalofuata ba*ba*. Nasema mwenyewe kimya kimya, *baba*. Natenganisha sauti ya kwanza /b/. Neno *baba* halianzi na sauti /m/ hivyo naonyesha kidole gumba chang chini..

**VIDOLE VIWILI** *(Kwa sababu hii inatoa hatua katika utaratibu wa kufundisha na jinsi ya kuendelea hatua inayofuata)*

Litaje neno kisha taja kila sauti kwa kadiri unavyo andika kila herufi ya neno baba.

**KIDOLE KIMOJA (Tumia sababu zilizotajwa kwenye kidole kimoja)**

Leo tutasoma silabi. Tutataja kila sauti kisha tutasoma silabi. Naweka kidole changu chini ya kila herufi na kutaja sauti ya kila herufi. /m/ /a/. kasha nakipitisha kidole changu chini ya silabi na kutaja sauti yote ya silabi *ma*

**VIDOLE VIWILI (Tumia sababu zilizotajwa kwenye vidole viwili)**

Nasoma kichwa cha somo na kisha najiuliza mwenyewe,

Je, kichwa cha somo kimetaja watu au vitu? Kama kimetaja, naandika mahala pangu.

Kisha najiuliza, je kichwa cha somo kinataja jambo lolote? Kama kimetaja, kisha naandika kilicho tajwa mahala pangu.

Mwishoni, najiuliza, je nadhani hadithi hii inahusu nini? Kisha naandika ninachofikiri katika sehemu yangu.

- **Mazoezi elekezi**

Mwezeshaji awambie washiriki kuwa mazoezi elekezi yana vitu viwili muhimu: *mrejesho endelevu na maelekezo ya ufundishaji na ujifunzaji.*

Mrejesho endelevu hurejea kwenye ufaulu wa mwanafunzi na uwezo wao wa uelewa na kwa mafanikio makubwa humfanya mwanafunzi kubadilika zaidi. Ili kufanikisha hili, walimu wanatakiwa kufanya yafuatayo ;

- Waoneshe wanafunzi kama uelewa wao ni sahihi au sio sahihi.
- Waeleze wanafunzi kwanini jibu lao ni sahihi au sio sahihi.
- Waeleze wanafunzi wakati wa kujifunza wamefanikiwa kupata nini na kipi hawajafanikiwa kukipata
- Wape motisha wanafunzi kuendeleza juhudi katika kujifunza

Waambie washiriki kuwa utaonesha kwa kufanya mrejesho endelezi, kama ifuatavyo:

Iwapo nitawambia wanafunzi wangu wasome neno ***kula***, lakini wakasoma bila usahihi, wanafunzi wengine wakatamka ***kura.*** Nitasema, "Hapana, hivyo siyo sahihi, unavyo tamka siyo ***kula***, unatamka **kura** kwa unakosea herufi **'r'**. Haya tutaje sauti moja moja kwa pamoja na kisha tulitamke neno lote haraharaka. Haya tujaribu."

Waeleze washiriki kuwa hii inamsaidia mwanafunzi kufahamu jinsi ya kuanza kutatua tatizo lake. Endapo nitasema, Hapana, haimsaidii mwanafunzi kufahamu zaidi ya alivyo kuwa anafahamu mwanzo, au ni jinsi gani agundue kosa.

Waambie washiriki kuwa ufundishaji na ujifunzaji saidizi unatumika kuwasaidia wanafunzi wakati :

- wanapojifunza stadi mpya au dhana mpya.
- Aina hii ya ufundishaji humwezesha mwanafunzi kupata jibu sahihi, ni msaada wa aina ya kipekee ambao huwaruhusu wanafunzi kusonga mbele na kuelekea kupata stadi mpya na viwango vya uelewa, hata hivyo ikumbukwe kuwa ufundishaji na ujifunzaji saidizi;
- Haubadili stadi inayo kusudiwa wakati wa kujifunza
- Inatoa usaidizi wa kutosha kuruhusu wanafunzi kumaliza kazi inayokusudiwa wakati wa kujifunza.
- Hutoa muongozo wa kumsaidia mwanafunzi katika utafutaji wa jibu sahihi.
- Ni utaratibu wa muda ambao hukoma wakati mwanafunzi anapoanza kujitegemea.

- **Mazoezi binafsi**


Waambie washiriki kuwa mazoezi binafsi yanampa mwanafunzi fursa ya kufanya mazoezi ya mambo ambayo wanajifunza. Baadhi ya wanafunzi

wanahitaji mazoezi kidogo, wengine wanahitaji mazoezi zaidi. Wanaojifunza lazima wasihusishwe kwanza na zoezi la kufanya peke yao mpaka waweze kukamilisha kazi peke yao. Hatutaki wafanye kazi isivyo sahihi.


- **Tathmini**

Waambie washiriki kuwa kabla ya kumaliza somo, walimu lazima watathmini uelewa wa wanafunzi. Jedwali lifuatalo linaonesha mfano wa njia zinazotumika katika kufanya tathmini

**Kielelezo 2: Jedwali la Tathmini**





Kama wanafunzi walio wengi hawawezi kuonesha kuwa wamejifunza stadi na dhana muhimu, mwalimu anatakiwa asiendelee na somo mbele zaidi, au asifikirie kuwa yuko nyuma ya wakati. Badala yake, mwalimu lazima asimame, atafakari, na atafute mbinu nyingine za kufundisha dhana hii. Kumbuka kutafakari juu ya kiwango cha ufundishaji na ujifunzaji, kutilia maanani kwenye ufundishaji na ujifunzaji na ubora wa ufundishaji na ujifunzaji.



**Ufupisho**

Waambie washiriki kuwa, utoaji wa maarifa mapya ambao umezingania mbinu sahihi za ufundishaji na ujifunzanji husaidia kuweka mazingira mazuri ambayo wanafunzi wanaweza kupata uelewa mpya. Walimu wanaweka mazingira mazuri ya kujifunzia kwa kuwapa wanafunzi msaada unaotakiwa ili kupata stadi na maarifa mapya na kuweka fursa nyingi ya kufanyia mazoezi. Katika mfumo, ujifunzaji unaonekana kama ni utaratibu elekezi na si zao la mwisho. Na hili linakuwa dhahiri kwa kufanya yafuatayo:

- Tunawaeleza wanafunzi matarajio yetu , na tunatoa mfano wa wazi.
- Tunafanya mazoezi pamoja na wanafunzi na tunawapa nafasi ya kufanya mazoezi juu ya walichojifunza kwa kujitegemea.
- Kama wanafanya makosa, tunatoa tathmini rasmi
- Tukiwa na uhakika kuwa wana uwezo wa kumaliza kazi, tunawapa fursa ya kutumia stadi kwenye mazingira mapya.



**Tafakuri**
**Kazi ya kufanya: Mapitio ya muda**
**Maelekezo ya kazi ya ufundishaji na ujifunzaji**

Wape nafasi washiriki kufikiria juu ya mazoezi ambayo tumeyazungumzia hapo awali, kisha wajifanyie tathmini wao wenyewe. Hawatakiwi kumshirikisha mtu yeyote juu ya tathmini yao, ila itawasaidia kuwaonesha wapo hatua ipi katika matumizi ya mazoezi

| Kazi | Siku zote inatumika | Inatumika kwa baadhi ya wakati | Kamwe hayatumiki | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| Maandalizi awali yanatolewa | | | | |
| kazi mfano | | | | |
| Mazoezi elekezi linatolewa | | | | |
| Tathmini endelevu inatolewa | | | | |
| Ujifunzaji saidizi | | | | |
| Hutoa mazoezi binafsi | | | | |
| Wanafunzi wanatathminiwa na kutumia taarifa za upimaji kupanga ufundishaji na ujifunzaji | | | | |

**Kazi ya kufanya: Kukamilisha kazi.**

Pitia majibu ya kazi pamoja na washiriki wa mafunzo. Maelekezo haya yanawasilishwa kwa kurudia rudia katika kiongozi cha mwalimu.

**Maelekezo**

- Andika maandalizi ya mazoezi ambayo utayatekeleza baada ya mafunzo haya.
- Andika swali 1 au 2 ambayo bado unayo kutokana na kipengele hiki
- Ruhusu dakika 3–5 zitumike kujadili maswali.

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

## Mazoezi zaidi ya Ufundishaji Mzuri (saa1)

Waambie washiriki kuwa utazungumzia zaidi kuhusu mazoezi ya ufundishaji mzuri kwa kulenga maeneo muhimu yafuatayo:

- Fursa ya kufanyia mazoezi stadi, na
- Kasi

Hapa dhana kuu mbili ni:

1) Kuwafanya wanafunzi washirki katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kufanya mazoezi.

2) Kutumia mbinu hizi, mwalimu anaweza kufanya tathmini endelezi

Kwa mfano: <u>Kufundisha katika mazingira ya darasa lenye wanafunzi wengi.</u>

Waeleze washiriki kuwa umuhimu wa muda katika kazi unatambulika kama kigezo muhimu cha kujifunzia. Katika Kujifunza, wanafunzi lazima watumie muda katika kushiriki katika kazi za kitaaluma. Katika kujenga usikivu wa mwanafunzi katika madarasa yenye wanafunzi wengi panahitajika maelekezo fasaha ya kuongoza mazoezi. Katika madarasa hayo fursa za wanafunzi kunufaika na maarifa yatolewayo, vifaa au kufanya mazoezi ya stadi zinayotolewa ni ndogo kama wanafunzi hawamsikii mwalimu.

## Njia bora za ziada za ufundishaji

Waambie washiriki kuwa njia bora ya ufundishaji lazima ikidhi malengo yafuatayo;

- Kuwapo kwa fursa ya wanafunzi kufanyia mazoezi stadi walizojifunza
- Kuwapo na kasi ya kufundishia na kujifunzia inayokubalika

Kuna njia tofauti za kuwafanya wanafunzi washiriki na wafanye mazoezi kwa pamoja. Miongoni mwa nJia hizi ni kuwafanya wanafunzi wajibu kwa pamoja badala ya kujibu mmoja mmoja. Kwa kutumia njia hii wanafunzi wanapata muda zaidi wa kufanyia mazoezi walichojifunza kuliko wakati mwanafunzi akifanya mmoja mmoja. Pia wanafunzi wanapata fursa ya kufanya mazoezi na kujibu maswali yote kwa pamoja. Kumbuka unapouliza swali na kumchagua mwanafunzi mmoja kujibu swali, ni mwanafunzi mmoja ambaye atakuwa amepata fursa ya kufanya mazoezi.

Hali kadharika, kama ukiuliza wanafunzi wote, inamaanisha kuwa wanafunzi wote watakuwa wamepata fursa ya kufanya mazoezi kwa pamoja.

**Fikiri- Jozisha:** Wanafunzi wakiwa kwenye jozi waambie kila mmoja kufikiri peke yake, halafu ashirikiane na jirani yake na kisha wakubaliane jibu lao. Kisha makundi wajadiliane na darasa lote kwa ujumla.

**Mgeukie jirani yako:** Wanafunzi wageukiane kumaliza kazi walizopewa.

**Majibu ya kadi:** Wanafunzi wakunje kadi zao, alama au vitu kwa wakati mmoja kuonesha jibu kwa maswali au tatizo. Wanafunzi wajibu kwa pamoja ili kuhakikisha wanashirikishwa katika nadharia zima ya utambuzi.

**Bana kadi**: Kadi zenye majibu kwenye kadi moja; wanafunzi wabane kadi yenye jibu sahihi.

**Majibu ya pamoja:** Wanafunzi wote wajibu kwa pamoja. Kama una darasa kubwa, baada ya wanafunzi kujibu, unaweza kutumia utaratibu wa kuligawa darasa kwa kuwaomba wanafunzi wa kike wajibu au wa kiume wajibu au wanafunzi waliokaa nyuma au mbele na kadhalika kujibu maswali yako ili uweze kutambua kwa urahisi wapi wameelewa na wapi hawajaelewa.


Mwisho, ikiwa wanafunzi wanajibu maswali kwenye vikundi, hakikisha kuwa kila mwanafunzi anashiriki kikamilifu kwa kuyatembelea makundi yote muda wote wa ufundishaji na ujifunzaji.

Fanya mazoezi na wanafunzi hadi hapo watakapokuwa wameelewa stadi. Lakini kama wanafunzi wako wanahitaji mazoezi ya ziada kuelewa stadi, endelea kuifanyia kazi hadi wanafunzi wote watakapoweza kusoma kwa ufasaha.

Matumizi ya michoro sanifu (graphic organizer) huwasaidia wanafunzi kutilia mkazo, kuelewa na kuunganisha taarifa. Pia wanatoa kifaa thabiti katika kuwasilisha mawazo na mahusiano yake.

**Kasi wakati wa ufundishaji na ujifunzaji**

Mazoezi mengine muhimu ya kujifunza na kasi ya kujifunza. Kazi ifuatayo inadhihirisha kasi ya kujifunza kwa mwanafunzi.



**Kazi ya kufanya: Kasi (haraka au taratibu) wakati wa ufundishaji na ujifunzaji**

**Maelekezo**

Waongoze washiriki kufikiria kuhusu wanafunzi walioko darasani. Washiriki waweze kubainisha wanafunzi ambao wanaweza kuwa na ugumu wa kujifunza endapo kasi ya ufundishaji na ujifunzaji ni ya haraka.Nini kinaweza kutokea? Andika kitu kimoja (1). (dakika 2)

Sasa fikiria kuhusu wanafunzi ambao kama kasi ya ufundishaji na ujifunzaji ni ya polepole watakuwa na ugumu kiasi gani. Nini kinaweza kutokea? Andika kitu kimoja (1). (dakika 2)

Waongoze washiriki 2–3 washirikiane majibu yao. Waulize kuhusu wanafunzi waliowafikiria na matokeo yake ya ufundishaji na ujifunzaji ambao ulikuwa wa kasi sana.
Baada ya washiriki wote kushirikiana majibu yao, waulize wengine katika kundi kama wameandika majibu sawa au yanayo fanana.

Kisha waulize washiriki wengine wa 2–3 watoe mawazo yao kuhusu wanafunzi ambao wasingefanya vizuri kama ufundishaji na ujifunzaji ungekuwa polepole sana. Baada ya wote kushirikiana katika majibu, waulize wengine katika kundi wanyoshe mikono yao kama wameandika kitu hicho hicho au kinacho fanana.

Mwezeshaji awaongoze washiriki kupitia baadhi ya mazoezi ambayo husaidia kuleta kasi nzuri wakati wa ufundishaji na ujifunzaji

- Uwe umejiandaa vizuri kufundisha somo. Hii inamsaidia mwalimu kuwa na kasi ya haraka ya kufundishia.
- Wanafunzi wote wanahitaji muda wa kufikiri baada ya mwalimu kuuliza swali. Hata hivyo, muda mwingi zaidi wa kufikiri unaweza kusababisha mwanafunzi kujenga tabia isiyo msaidia mwanafunzi kujifunza.
- Ili kuwa na kasi nzuri mazoezi yanahitajika. Mwalimu lazima afanye mazoezi ya kusoma somo kwa sauti kabla ya kufundisha.
- Wanafunzi wanaojifunza taratibu wanakusanya taarifa kwa kasi ya taratibu. Kuongeza kasi ya kutoa jibu inawasaidia wanafunzi kukusanaya taarifa za majibu kwa kasi zaidi.
- Kadiri wanafunzi wanavyokuwa mahiri katika malengo, walimu lazima waongeze kasi ya shughuli. Rekebisha kasi ya ufundishaji na ujifunzaji ilikuwahusisha wanafunzi na kuwapa changamoto wakati wanajenga umahiri wa kila shughuli.
- Mwalimu lazima aendelee na somo iwapo wanafunzi wengi wanaonyesha umahiri wao, asi ende kasi ya haraka haraka wala ya polepole, ila atoe msaada wa ziada kwa wale wanaohitaji.

Muda wa kusubiri utabadirika kutegemeana na shughuli husika. Wanafunzi wanapo jifunza stadi kwa mara ya kwanza, wanahitaji muda zaidi wa kufikiri ili watoe majibu kwa usahihi zaidi. Punguza muda wa kusubiri kadiri wanafunzi wanavyo fanya marudio.

Waambie washiriki kuwa utaonyesha mfano wa jinsi ya kufundisha kwa "kasi ya kujiamini" na uwapatie wanafunzi wote fursa ya kufanya mazoezi.

**Silabi : Utaratibu wa usomaji**

**STADI: Usomaji wa silabi**

**LENGO: baada ya kuoneshwa silabi, wanafunzi watasoma silabi zilizoundwa kwa herufi walizokwisha jifunza.**.

**Maandalizi awali**

***Mwalimu:*** Tutatumia sauti tunazo zijua kusoma silabi. Tutatamka kila sauti kisha tutasoma silabi. Nitaonyesha kidole changu chini ya kila herufi na mtatamka sauti ya herufi. Baada ya kutamka sauti zote za silabi., nitapitisha kidole changu chini ya silabi na ninyi mtaitaja.

**Kazi mfano:**

*Weka mkono chini ya herufi ya kwanza ya silabi ubaoni na kusema* ,

***Mwalimu:*** Nitazame mimi, m a - ma, m e -me, m i - mi.

**Mazoezi elekezi:**

***Mwalimu:*** Sasa tutafanye pamoja. Kumbuka kutaja sauti ya kila herufi wakati naoneshea kidole.

*Mwalimu anaonyesha kwenye kila herufi ya silabi ubaoni.*

***Mwalimu na wanafunzi:*** m a - ma, m e -me, m i - mi.

**Mazoezi binafsi:**

***Mwalimu:*** Sasa jaribu.

**Wanafunzi:** Taja herufi zifuatavyo bila kusaidiwa na mwalimu. m a - ma, m e - me, m i - mi..

**Tathmini endelezi:** Endelea kufanya mazoezi na silabi zaidi.

Waulize washiriki kama wana maoni yoyote au maswali kabla hujaendelea?

## Hitimisho

- Waeleze washiriki kuwa masomo yote ambayo wameyaangalia siku ya leo yana vipengele vinavyojirudia. Masomo haya yana chimbuko la nadharia ya usomaji na kutambua kuwa watoto ni wanaushirika hai katika kujifunza kwao, na kwahiyo lazima wahusishwe kiutambuzi katika mchakato wa kujifunza. Somo hili linahusisha vipengele vifuatavyo:
- Maelekezo ni <u>shirikishi na yenye vitendo vya kasi</u> (bila kuwaacha wanafunzi wengi) ili kujihakikishia kuwa uhusika hai wa wanafunzi upo tangu mwanzo hadi mwisho wa somo;
- Ufundishaji unafanywa kwa hatua ndogo ndogo, huku wanafunzi wakifanyia mazoezi kila hatua kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wanapata mafanikio ya hali ya juu; na

- Wanafunzi wanapatiwa fursa ya kukazia maarifa ambacho wanajifunza katika mazingira mengine.

Kwa nyongeza, masomo hubadilika, masomo ya utangulizi wa dhana au stadi mpya huongozwa na mwalimu wakati mazoezi na majumuisho ya taratibu za kila siku yanamlenga mwanafunzi. Kumbuka mzunguko wa maelekezo; utangulizi, mazoezi na majumuisho.

Waambie washiriki kuwa kuchanganya hatua hizi kunamuwezesha mwalimu kutoa uwajibikaji kwenda kwa mwanafunzi na kutoa fursa kwa mwanafunzi kufanya mazoezi na kujumuisha yale anayojifunza. Hali kadhalika, waambie washiriki kuwa hupata stadi na maarifa yanayohitajika kwa sababu maelekezo yanapangwa kwa mawanda ambayo hutanguliza stadi kimantiki.

Waambie washiriki kuwa utatoa mfano wa somo na wao wataigiza kuwa wanafunzi. Wafahamishe kuwa ukisha toa somo la mfano, wao watakaa katika vikundi na mwanakikundi mmoja atafundisha somo hilo hilo.

**Majumuisho**

Waambie washiriki kuwa kuna mazoezi mengi yanayoweza kutumika kuongeza ushiriki wa mwanafunzi katika kujifunza. mazoezi yenye ufanisi lazima yawe na lengo maalum, na humpa kila mwanafunzi kazi ya kufanya na kwa kasi ya kuridhisha.

Katika kuhakikisha ushiriki wa mwanafunzi ni mzuri, mwalimu ahakikishe kuwa muda wa ufundishaji unatumika vizuri na wanafunzi wanajifunza kwa juhudi.


Masomo yanayowafanya wanafunzi wajibidishe yanapaswa kuwa na vipengele vifuatavyo:

- Ufundishaji ni shirikishi na wenye kasi (lakini si wa haraka kwa wanafunzi wengi) kuhakikisha wanafunzi wako muda wote katika kazi wakati wote wa kipindi.
- Ufundishaji unatolewa katika hatua ndogo ndogo, wanafunzi wanafanya mazoezi kila baada ya hatua fulani ili kuhakikisha wanapata mafanikio ya hali ya juu,
- Wanafunzi wanapewa nafasi za kutumia kile wanajifunza katika muktadha tofauti

Kwa kuongezea, masomo yanatofautiana katika ufindishaji na ujifunzaji. Mathalani, masomo yanayotoa utangulizi wa dhana mpya au stadi na yanamlenga mwalimu wakati wa mazoezi na majumlisho wakati wote yanawalenga wanfunzi wenyewe.

**Stadi: Utabiri**
**Lengo la kujifunza:** Kabla ya kusoma matini, mwanafunzi atatumia kichwa cha habari kutabiri kitakachojiri katika habari
**Maandalizi awali**: Tambulisha kile ambacho mwanafunzi atafanya, kile anachotakiwa kujaribu katika kujifunza.
**Mwalimu:** "Leo tutasoma hadithi na tutabashiri nini kitakachotokea kwenye hadithi". Utabiri ni matarajio yanayojengwa juu ya taarifa chache tulizonazo tayari kuhusu hadithi yenyewe.
Tunaweza kutabiri kwa kuzingatia kichwa cha habari na picha. Tunaweza kusoma kichwa cha habari na kufikiri nini kinasimuliwa na tunaweza kuangalia picha na kufikiri kila picha inamaanisha nini na nani yumo katika picha na kitu gani kinatokea.
Tutatumia taarifa kufanya utabiri kuhusiana na hadithi na nini kinaweza tokea. Tukishamaliza hadithi tutarudi nyuma na kuangalia kama utabiri wetu ulikuwa sahihi.
**kazi mfano**: Soma kichwa cha habari,kisha uliza maswali yafuatayo;
**Mwalimu**: :
"Ninasoma kichwa cha habari na kisha najiuliza mwenyewe"
Je, kichwa cha habari kinataja watu au vitu?
Je, kichwa cha habari kinataja tukio?
Je, nafikiri hadithi inazungumzia nini?
**Mazoezi elekezi**: Waoneshe wanafunzi kichwa cha habari cha kitabu au hadithi na sema yafuatayo:
**Mwalimu**: 'sasa tutafanya kazi hizi sote kwa pamoja ''.Tutaangalia kichwa cha habari na kuuliza kila swali. Je, kichwa cha habari kinataja watu au vitu?"
**Mwalimu na mwanafunzi**: Wanajibu swali.
**Mwalimu:** '' Sasa tutatoa utabiri." Fanya kazi na mwenzako/kikundi na mtoe utabiri.
**Mazoezi binafsi**: Waruhusu/wawezeshe wanafunzi kufanya wao wenyewe kwa kujitegemea.
**Mwalimu**: Sasa utafanya utabiri na mwezako au kikundi, utauliza swali na kukamilisha maandalizi awali.
**Mwanafunzi**: Geuka kwa mwezako kujibu swali na andika majibu.
**Mwalimu**: Ataita wanafunzi kati ya (3-4) kuwasilisha utabiri wao na kutoa maoni kwa kila utabiri -Je, utabiri unazingatia kilichomo kwenye kichwa cha habari? Je, utabiri utafanyika kirahisi?
Baada ya kusoma hadithi, mwalimu anarudi na kuhakikisha kama utabiri ulikuwa sahihi au hapana.
**Matumizi**: wanafunzi wanakumbushwa kutumia maswali wakati wanapotabiri na wakati wanaposoma hadithi.

Mwisho,wanafunzi wanapata stadi na maarifa yanayotakiwa kwa sababu ufundishaji na ujifunzaji umepangiliwa na hufuata mtiririko katika kutambulisha stadi inayokusudiwa kwa somo husika na kufuata utaratibu utaratibu mzuri.



**Kazi ya kufanya: Ufahamu wa somo la utabiri**
Sasa tutalipitia somo linalohusiana na utabiri linalozingatia mazoezi yote ambayo yamewasilishwa mwanzoni. Tafadhari uwasilishaji wa somo hili uwe makini wa hali ya juu. Baadaye, mtakaa katika makundi na mwanafunzi mmoja kutoka katika kila kundi atafundisha somo kwa kutumia muundo huu tuliotumia kufundishana.

**MFALME WA PORI**



**Vipengele muhimu katika somo la utabiri ni kama vifuatavyo:**
Waambie washiriki kuwa wakati unafundisha somo la utabiri, kuna vipengele kadhaa muhimu vya kuzingatia huku tukikumbuka kumsaidia mwanafunzi:
Utabiri lazima uwe na mantiki, hii inamaananisha kuwa utabiri uzingatie kile kilichowasilishwa, je ni kichwa cha habari, jalada la kitabu au ufafanuzi. Inabidi vihakikishwe mara baada ya kusomwa.

Kama mwanafunzi anafanya utabiri ambao unaonekana hauna mantiki, muulize aeleze sababu anayoitumia, kisha msaidie kujenga uelewa wenye mantiki kwake, na kumsaidia kufanya masahihisho. Hakikisha unataja kitu kizuri kuhusu utabiri, msaidie mwanafunzi kuunganisha picha kwa kile wanachokijua na kile wasichokijua.

Wanafunzi wanapaswa kuelewa hakuna tatizo kama utabiri wao haukuwa sahihi

Unaweza kujenga uelewa wa kimantiki kwa mwanafunzi, na kukamsaidia kufanya masahihisho. Hakikisha unataja kitu kizuri kuhusu utabiri alioutoa, aidha msaidie mwanafunzi kuunganisha picha kwa kile anachokifahamu na kile asichokifahamu.

**Kazi ya kufanya: Mazoezi**
**Maelekezo kuhusu kazi ya kufanya:**
Wagawe washiriki katika makundi ya watu 10. Katika Kila kundi mmoja wenu atakuwa mwalimu na wengine watakuwa wanafunzi. Muundo wa somo lililopita utatumika kama muongozo kuuliza swali kuhusu jalada la kitabu kwenye ukurasa unaofuata.

**USAFI WA MIKONO**



**Ufupisho**
Wakumbushe washiriki kuwa kabla ya kufikiria kuhusu ufundishaji wa kusoma, ni muhimu kufahamu jinsi wanafunzi wanavyojifunza. Sisi kama walimu tunapaswa kuhakikisha kuwa utaratibu wa kujifunza unaendeshwa kwa uwazi na kwa utaratibu.

Kama tulivyobaini katika kipindi kilichopita, mfumo wa ufundishaji unafafanua ni aina gani ya mafunzo yanayohitajika. Hii inahusu uanzishwaji wa stadi mpya au mbinu mpya, mazoezi na majumuisho.

Kupitia masomo haya matatu, kuna utaratibu unaowasaidia walimu kutengeneza mazingira ya kujifunzia kama vile: maandalizi ya awali, kutoa mifano, mazoezi elekezi na tathmini ya mara kwa mara. Kwa kutumia utaratibu huu kujifunza huonekana kama mchakato/mfumo na siyo kama zao la mchakato wenyewe.

## SIKU YA PILI

**Mapitio ya mawasilisho ya siku iliyotangulia (dakika 30)**


***Swali la marudio***

Wakaribishe washiriki. Waambie utaanza siku kwa kupitia somo lililowasilishwa siku iliyotangulia na kujibu maswali ya somo la siku lililotangulia.

**Kazi ya kufanya: mapitio ya mafunzo**.

***Maelekezo kuhusu kazi ya kufanya***:

Mwezeshaji na washiriki wapitie maelekezo ya kazi ifuatayo pamoja na washiriki wa mafunzo. Maelekezo haya yanawasilishwa kwa kurudiwa rudiwa katika kitini cha mwalimu.



**Mwezeshaji awaongoze washiriki kujibu maswali yafuatayo (umepewa majibu kama mwezeshaji):**

- **Zipi ni aina 3 za masomo**? (Jawabu : utangulizi, mazoezi na majumuisho)
- **Vipi ni vipengele 2 vya mazoezi elekezi?** (Jawabu: mrejesho wa mara kwa mara na ufundishaji na ujifunzaji saidizi)
- **Zipi ni njia 2 za kuonesha mfano?** (Jawabu: kazi na kufuata hatua kwa hatua)
- **Nini lengo la maandalizi awali?** (Jawabu: Kuwapa wanafunzi taarifa kuhusu atakachojifunza na kuwaandaa kuwa tayari kujifunza)
- **Ni wakati gani unatoa mazoezi binafsi?** (Jawabu: Wanafunzi wanapokuwa wameanza kuzimudu stadi au maarifa mapya)
- **Nini lengo la tathmini?** (Jawabu: Kutafuta kama wanafunzi walio wengi wamepokea kile kilichokuwa kinafundishwa. Na kama bado, husaidia katika kuamua ni aina gani ya ufundishaji mzuri unahitajika, na kama walio wengi wamepata maarifa lengwa, husaidia kuamua kama wanafunzi fulani wanahitaji msaada au mazoezi ya ziada)
- **Ni kwa namna gani unafikia uamuzi wa kipi kibadilishwe katika ufundishaji wako? (**Jawabu: kama wanafunzi hawakupokea maarifa yaliyotarajiwa, zingatia ufundishaji katika 1. Kiwango 2. Mwelekeo 3. Ubora )




**Utangulizi kuhusu ufundishaji wa kusoma (dakika 30)**
**Umuhimu wa kujifunza kusoma mapema**


Matokeo ya tafiti mbalimbali yanaonesha faida kadhaa kuhusu umuhimu wa kujifunza kusoma mapema. Baadhi ya faida zake ni kama zifuatazo:

- Matokeo mazuri kitaaluma
- Stadi za msingi katika kuzungumza
- Misingi ya usomaji wa kitabu
- Stadi nzuri za mawasiliano

- Kuimudu lugha
- Stadi zaidi za kufikiri (kimpangilio)
- Ufahamu kuwa kusoma ni burudani au furaha

Waelekeze washiriki kuwa, kama walimu tunapaswa kufahamu kuwa wanafunzi kama hawapati stadi za kusoma mapema, ni dhahiri kuwa watakuwa nyuma ukilinganisha na wenzao katika makundi- rika yao. Sababu za kuhimiza wanafunzi wajue kusoma mapema ni pamoja na:

- Njia za kupata elimu zinaanzishwa mapema katika makuzi ya mtoto
- Wanafunzi wanaoanza na njia duni au isiyioridhisha huendelea na njia hiyo mpaka mwalimu atakapobadilisha mfumo wa ufundishaji na ujifunzaji.
- Kadiri tunavyochelewa kubadi mfumo wa ufundishaji, ndivyo inavyokuwa vigumu kwa wanafunzi kubadii njia yao ya kujifunza kwani maudhui ya kile wanachojifunza huzidi kuwa magumu na yasiyoeleweka.



**Kazi ya kufanya**: **kusoma kwa lengo la kujifunza**
Katika makundi ya watu 5-10 washiriki wajadili nafasi ambayo wanafunzi huweza kuwa nayo baadaye au kile watakachoweza kukifanikisha kama wakiweza kusoma ukilinganisha na wale wasioweza kusoma.

## Maelezo ya jumla kuhusu vipengele vitano muhimu katika kusoma (dakika 30)

*".......kuna vipengele vitano vya msingi katika kusoma. Vipengele hivi ni stadi na ufahamu ambavyo wanafunzi wanahitaji ili kuwa wasomaji wazuri. Stadi zote hizi lazima ziende pamoja ili kuwawezesha wanafunzi kusoma na kupata maana kutoka katika matini waliyosoma. Yawezekana ukawa tayari unavifahamu na kuvitumia katika ufundishaji wako, hata hivyo, ni muhimu kukielewa kila kipengele na umuhimu wake ili kuweza kusoma."*

Mwenzeshaji atoe atoe ufafanuzi kwa kila kipengele na awaongoze washirki kutoa mfano kwa kila kimoja. Kama wakipata ugumu katika kutoa mifano, wape mifano.

Utafiti wa kisayansi unaonesha wazi kuwa ufundishaji makini wa kusoma unazingatia maeneo muhimu matano:

Utambuzi wa umbosauti – kuelewa kuwa maneno yanaundwa na sauti, kwa mfano, neno baba linaundwa na sauti mbili: ba-ba; na kuweza kuzipanga vizuri sauti hizo ili kuunda maneno (kwa mfano kuelewa kuwa maneno baba au babu yote huanza kwa sauti ileile).

Utambuzi wa fonimu (kipengele kidogo katika ufahamu wa umbosauti) – kinahusu uwezo wa kusikia, kuzitambua na kuzitumia sauti – fonimu – katika lugha ya mazungumzo.
(mfano : baba – ba ba), (ba –/b/ /a/), (baba - /b/ /a/ /b/ /a/)
Fonetiki – kuelewa kuwa herufi huwakilisha vitamkwa/sauti na kuwa maneno huundwa na vitamkwa na herufi hizo.

Ufasaha – kusoma au kuzitambua herufi na maneno kwa haraka na kwa usahihi(katika hali ya kawaida.

Msamiati – kutoa maana ya maneno katika lugha..

Ufahamu - kutoa tafsiri ya maneno yaliyomo katika habari.*Vipengele hivi 5 vitajenga msingi katika programu ya kusoma na vitafafanuliwa kwa kina katika mada itakayofuata..*

## Vipengele vitano muhimu katika ufundishaji wa kusoma




**Utambuzi wa umbosauti (saa1.5)**
**Vifaa/zana: Orodha ya maneno**
Wambie washiriki kuwa, kipengele cha kwanza ni utambuzi wa umbo sauti. Kipengele hiki ni moja ya stadi za awali na ufahamu wanaouhitaji wanafunzi ili kujifunza kutamka au kutafsiri maneno.
**Ufafanuzi**: Uwezo wa kusikia, kuzitambua na kuzitumia sauti katika maneno ya kusemwa/kutamkwa.

### Umuhimu wa kutambua umbo sauti


- Huwawezesha wanafunzi kuyatenga maneno katika vitamkwa (vipande sauti), kuunganisha vitamkwa ili kuunda maneno na kutumia vitamkwa hivyo kwa kuviongeza au kuvipunguza kutoka katika neno kulingana na kile anachojifunza.
- Kuzingatia utamkaji ni stadi halisi ya kuzungumza ambayo hutakiwa kufundishwa pasipo kutumia maandishi.

**Umuhimu wake katika kusoma**

- Watoto wanahitaji kuzifahamu sauti zilizo katika maneno ili waweze kuziweka sauti/fonimu hizo katika maandishi(herufi) na kuweza kupata kanuni ya kialfabeti.
- Kuunganisha na kutenganisha vitamkwa/sauti husaidia kufanikisha usomaji.

**Toa mifano kwa kila kipengele na kisha jadiliana na washiriki.**
Katika kipengele cha kuzingatia umbosauti kimo kipengele kidogo cha kuzingatia fonimu. Katika kufundisha uzingatiaji wa fonimu, mwalimu huwasaidia wanafunzi kuzisikia sauti zinavyotamkwa katika maneno na kufanya mazoezi ya stadi za kuunda maneno kwa kutumia fonimu hizo.


**Utaratibu wa kufundisha: Jinsi ya kufundisha uzingatiaji wa umbosauti**
**Maandalizi awali:** Nini wanafunzi watajifunza na umuhimu wake.
**Mwalimu: "**Tunafahamu kuwa sentensi huundwa na maneno na maneno huundwa na vitamkwa/sauti[uzingatiaji wa matamshi] na sauti/vitamkwa huundwa na fonimu[uzingatiaji wa sauti]. Leo tutafanyia mazoezi utamkaji wa sauti zikiwa katika maneno na kuunganisha sauti ili kuunda maneno.
**Kazi mfano [ninatenda]**: mwezeshaji atatoa mfano wa jinsi ya kuzingatia matamshi kisha huacha ili kujadiliana na washiriki wa mafunzo.
**Mwalimu**: sikiliza neno hili *mama* na nitakwambia kitamkwa(sauti) unachokisikia katika neno *mama.*
*Mwalimu anatamka neno 'mama' polepole na kuwambia wanafunzi kuwa kitamkwa cha kwanza katika neno hili ni /m/.*



**Kazi ya kufanya: mapitio na mazoezi**
Mwezeshaji awaongoze washiriki kucheza igizo - dhima wakivaa uhusika wa wanafunzi. Mwezeshaji atawaongoza, walimu kubainisha na kuvitambua vitamkwa vilivyowasilishwa na mwezeshaji.


**Mazoezi elekezi [tunatenda]:** Mshiriki anatakiwa kuelezea vipengele viwili katika mazoezi elekezi yaani mrejesho rasmi na ufundishaji saidizi kwa kurejelea kipindi kilichotangulia. Katika kulifanyia mazoezi ili liwe na manufaa washiriki (waliovaa uhusika wa uanafunzi) wafanye makosa ili mwalimu afanye mazoezi ya kutoa mrejesho rasmi.

**Mwalimu:** Ndiyo, /m/ ni kitamkwa cha kwanza katika neno *mama*. Nitajie kitamkwa cha kwanza katika neno *maji.*
Mwalimu na mwanafunzi: **/m/**



**Kazi ya kufanya: Igizo-dhima**
Washiriki wanatakiwa kugawanyika katika vikundi vidogovidogo na kufanya mazoezi ya uzingatiaji wa umbosauti. Kila mshiriki katika kikundi lazima apate nafasi ya kuwa mwalimu angalau mara moja.

**Mazoezi binafsi [unatenda]:** washiriki katika vikundi vyao hufanya mazoezi yanayojirudia ili kupata ishara namna utambuzi wa fonimu kwa mwanafunzi unavyojengeka.
**Mwalimu:** Kipi ni kitamkwa cha kwanza katika neno *baba*?
**Wanafunzi:** /b/.
**Mwalimu:** Ni sauti gani huweza kuundwa kwa kuunganisha vitamkwa/ sauti *b* na *a*?
**Wanafunzi:** ba.
**Mwalimu:** Ni neno gani huweza kuundwa kwa kuunganisha vitamkwa */b/ /a/ /t/ /a/?*
**Wanafunzi:** bata**.**
**Mwalimu:** Tamka neno *baba* kisha badili kitamkwa /b/ na nafasi yake weka /s/.
**Wanafunzi:** saba.
**Mwalimu:** Onesha ni vitamkwa vingapi vimo katika neno *bata*.
**Wanafunzi**: 4 - */b/ /a/ /t/ /a/.*



**Kazi ya kufanya: Igizo-dhima**
Washiriki wafuatishe mfano wa mwezeshaji na kisha watafanya mazoezi kwa kutumia igizo-dhima. Kazi zitarajiwazo wakati wa igizo-dhima:

- Kuunganisha vitamkwa kuunda sauti.
- Kuunganisha vitamkwa au sauti ili kuunda maneno.
- Kutenga maneno katika vitamkwa au sauti.

**Mfumosauti/fonetiki**

**Vifaa/zana:** herufi, silabi na kadi za maneno/orodha ya silabi na maneno.

Mwenzeshaji awambie washiriki kuwa, hiki ni kipengele cha pili kilicho na stadi mbalimbali ndani yake. Stadi hizi zinahusiana kwa kuwa herufi ni alama za kuonekana za sauti na alama hizo hutumika katika kuandika maneno.
Stadi hii huwataka wanafunzi kufahamu jinsi sauti na herufi zinavyohusiana na jinsi ya kuyatenga maneno yaliyoandikwa katika vipande-sauti vidogo

vidogo kama vile silabi au herufi ili kutamka maneno. Ufahamu huu ndio unaohitajika ili wanafunzi waweze kusoma.
"*mara nyingi kanuni za alfabeti hufundishwa kwa kutumia mbinu ambayo kwa kawaida hufahamika kama mfumo sauti"*

**Ufafanuzi wa mfumosauti:** Ni njia ya ufundishaji wa kusoma ambayo hufundisha mahusiano yaliyopo baina ya herufi na sauti na mbinu za kutumia mahusiano hayo katika kusoma maneno.

**Umuhimu wa fonetiki katika kusoma.**

- Ndio msingi wa baadaye kwa stadi za kusoma na kuandika .
- Huwapa wanafunzi njia za kutamka na kusoma maneno ambayo bado hawajayafahamu Wanafunzi wanahitaji kujifunza jinsi ya kutenga na kuunganisha vitamkwa na kutumia maarifa hayo katika kusoma na kutaja herufi mojamoja za maneno. hii ndiyo tunaita fonetiki.
- Wanahitaji pia kupata fursa ya kusoma maneno ili kwamba kitendo cha kuyasoma kigeuke kuwa cha utaratibu wa kawaida.

**Utaratibu wa kufundisha: Jinsi ya kufundisha fonetiki**
**Maandalizi awali**: wanafunza watajifunza nini na umuhimu wake ni upi katika kuimarisha stadi ya kusoma?

**Mwalimu**: "tutajifunza kitamkwa kipya na herufi tunayoitumia kukiandika kitamkwa hicho. Hii itatusaidia kuweza kuyasoma maneno yaliyo na kitamkwa hicho."
**Kazi mfano[ninatenda]:** Washiriki watamsikiliza mwezeshaji atakapokuwa akitoa mifano kuhusu jinsi ya kufundishwa vitamkwa kisha watajadili kuhusu kazi za kawaida wakati kuonesha mifano.
**Mwalimu**: kitamkwa chetu kipya ni /b/. Sikiliza maneno haya ili kubaini kitamkwa /b/.
*Mwalimu anatamka kila neno taratibu akitilia mkazo kitamkwa cha mwanzo katika kila neno*.
baba bibi bata bibo

**Marudio na mazoezi ya kazi za ufundishaji**
Mwezeshaji aoneshe mifano kwa kila kazi. Awaongoze washiriki kuwa makini kwenye utaratibu wa kufundishia na vipengele vingine vya ufundishaji. Mwezeshaji awaongoze washiriki waigize igizo dhima kwa kuvaa uhusika wa wanafunzi. Mwezeshaji akaribishe maswali kutoka kwa washiriki.

Hakikisha kuwa washiriki wameelewa vema stadi na kuzingatia stadi ya kuunganisha maneno inayoweza kuwa na ugumu kwa baadhi yao**.**

- Kuzitambua na kuzitaja herufi.
- Kuzibaini herufi na sauti zinazowakilishwa.
- Kuunganisha silabi.
- Kutaja vitamkwa katika maneno.
- Kuunganisha maneno.

Washiriki watamsikiliza mwezeshaji atakapokuwa anatoa mifano ya jinsi ya kufundisha sauti kisha watafanya mazoezi kwa pamoja na mwezeshaji


**Mazoezi elekezi [tunatenda]: Waongoze** washiriki wasome kwa pamoja mara 1-2. Wakati wa mapitio na mazoezi Ni vema kila mshiriki kuelewa vema stadi zifuatazo:

- Kuzitambua na kuzitaja herufi.
- Kuzibaini sauti za herufi zinazowakilishwa.
- Kuunganisha silabi.
- Kutaja vitamkwa katika maneno.
- Kuunganisha maneno.

**Mwalimu: "**Kumbuka, tunapoona herufi '**m'** siku zote huwakilisha kitamkwa au sauti /m/. Sikiliza maneno haya kisha bainisha ni neno lipi linaloanza na kitamkwa /**m**/."

Mwalimu anatamka maneno mawili: **mama, baba, bata, maji**.

**Wanafunzi**: *mama, maji*. Mwalimu anaandika ubaoni maneno: **mama, maji**




**Kazi ya kufanya: Igizo-dhima**

Mwezeshaji awagawe washiriki katika makundi na kufanya mazoezi mbalimbali kwa pamoja kila mmoja akitoa majibu sahihi juu ya stadi zifuatazo:

- Kuzitambua na kuzitaja herufi.
- Kuzibaini sauti za herufi zinazowakilishwa.
- Kuunganisha silabi.
- Kutaja vitamkwa katika maneno.
- Kuunganisha maneno.

Kisha washiriki wataonesha kila kazi kwa washiriki wote na kuruhusu washiriki kutoa maoni. Katika muktadha huu, herufi mwambatano zitafundishwa kama sauti moja na kuungana na irabu, wakati konsonanti zitaungana na irabu zitatumika kuunda silabi.

**Mazoezi binafsi [unatenda]**: Hii huwapa washiriki nafasi ya kufanyia mazoezi kile walichojifunza.



**Kazi ya kufanya: Tathmini ya mara kwa mara**.
Washiriki watajibu maswali kutoka kwa mwezeshaji katika kutathmini kama wengi wao wamepata stadi muhimu kabla ya mwezeshaji kendelea mbele. Kila mshiriki afanye pekee yake kuhusu:

- Kubainisha majina ya herufi
- Kubainisha sauti za herufi.
- Kuunganisha silabi.
- Kutaja vitamkwa.
- Kuunganisha maneno.

**Mwalimu**: "Sasa turudi nyuma tuone tulichojifunza. Tulijifunza kuwa herufi '**m'** inaweza kuwakilishwa na kitamkwa sauti /m/. Aidha, tulijifunza jinsi ya kutumia maarifa tuliyonayo kuhusu sauti ya herufi hiyo kutamka neno jipya.
Mwalimu anaandika maneno yanayoanza na '***m'*** na kuwaongoza wanafunzi wayasome yale yanayosomeka na kueleweka. Hii hutoa nafasi ya kubaini mwanafunzi mwenye uwezo wa kutumia uhusiano uliopo baina ya herufi na sauti katika maneno wasiyoyamudu bado.




**Ufasaha (saa 1.30)**
**Vifaa/zana: kadi za maneno/orodha ya maneno.**
Mwezeshaji awambie washiriki kuwa, kipengele cha tatu ni katika mtiririko wa vipengele vitano vya usomaji ni ufasaha. Hiki ni kipengele muhimu katika kuwawezesha wanafunzi kupata maana kutoka matini iliyosomwa. Wanafunzi wanatakiwa kuzitambua herufi na kuyasoma maneno kwa haraka na kwa usahihi ili kuweza kutumia muda wao na juhudi katika kupata maana za maneno kuliko sauti za kila herufi. Ni wazi kuwa wanafunzi watafanya mazoezi ya kusoma na kuandika kwa haraka na kwa usahihi wakati wote wa kuboresha ukuzaji wa stadi ya ufasaha.

**Ufafanuzi**: kusoma kwa ufasaha, kwa kasi, kwa hisia na kwa ufahamu.
**Umuhimu wa ufasaha katika usomaji**

- Usomaji unapokuwa wa moja kwa moja huuweka huru mfumo wa utambuzi kwa ajili ya ufahamu.
- Wanafunzi watakuza stadi ya ufasaha kupitiana kazi za marudio. Kazi zifuatazo zitamsaidia mwanafunzi kuweza kusoma kwa ufasaha:
- Kuzirudiarudia herufi, silabi, na maneno kila siku na kwa muda wa ziada siku ya Ijumaa.
- Michezo ya kusoma kwa ufasaha( Muongozo wa Mwalimu wa Ufundishaji kusoma).

**Utaratibu wa kufundisha:** Jinsi ya kufundisha ufasaha.

**Maandalizi awali:** Eleza nini mwanafunzi atakachojifunza na umuhimu wake.
**Mwalimu: "**Ninaposoma habari yoyote, kwa hakika ninataka kuelewa, wakati mwingine nitakisoma tena na tena. Kwa kufanya mazoezi ya mara kwa mara ninaweza kusoma kwa haraka na uelewa zaidi."

**Kazi mfano [ninatenda]:** Mwalimu anafafanua nini mwanafunzi atakachofanya.
Kipindi kinaanza kwa kufanya mapitio ya mada iliyotangulia. Marudio haya yanapita katika hatua zifuatazo: katika somo lililotangulia, mwalimu alisisitiza wanafunzi kuhusu kasi ya kusoma herufi, silabi,na orodha ya maneno pasipo kukosea. Ilifuata hatua ya kusoma sentensi mojamoja kwa kurudiarudia na kwa haraka wakati wote.
Mazoezi haya yanahitimishwa kwa wanafunzi kusoma aya kwa kurudia ili kukuza stadi ya kusoma kwa ufahamu. Zaidi ya hayo, somo lilitilia mkazo kusoma kwa haraka.
Baada ya mapitio ya somo la ufasaha mwalimu atawashirikisha wanafunzi kwa kutumia uzoefu wake katika mazoezi ya ufasaha kabla ya kuonesha kile kinachotarajiwa katika kipindi cha siku hiyo.

**Mwalimu**: "Leo, nitasoma herufi/silabi/neno/hadithi/sentensi ili muweze kusikia inavyotakiwa kutamkwa. Kisha mtapata fursa ya kufanya mazoezi ya kusoma wenyewe. Ninataka muwe na uwezo wa kuisoma kwa sauti na kwa haraka, kwa usahihi na kwa ufahamu; kama ninavyowasomea.

**Mazoezi elekezi [tunatenda]**
**Mwalimu: "**Katika kipindi hiki ninataka mfanye yafuatayo: Kwanza nataka ujisomee kwa kunong'ona. Nitakuja karibu na kusikilza kile unachokisoma, utatakiwa kusoma kwa sauti nitakapokuwa nakusikiliza lakini utarejea kwenye kunong'ona mara nitakapoenda kwa mtu mwingine."


Mwalimu anawapitia wanafunzi mmoja baada ya mwingine kusikiliza kasi ya kusoma na ufasaha katika kubainisha neno, upangaji wa maneno kwenye sentensi yenye maana; na kusoma kwa ufahamu kama kwenye kauli ya kuzungumza. Masahihisho ya makosa katika tafsiri ya neno hutolewa haraka ili wanafunzi walenge katika kukuza ufasaha.

Baada ya kuwasikiliza wanafunzi wote katika kikundi, mwalimu awahamisha huku akimuacha mmoja tu katika sehemu ya kusikiliza ili

kuendelea kufanyia mazoezi stadi ya kusoma kwa ufasaha. Mwanafunzi aliyebaki atasoma herufi/silabi/neno huku mwalimu akihesabu makosa na kukokotoa "maneno sahihi kwa dakika." Idadi inayopatikana hurekodiwa ili kumwezesha mwalimu kuendelea kufuatilia maendeleo ya mwanafunzi huyo katika kumudu stadi ya mtiririko fasaha. Taarifa hizi hukusanywa kwa kila mwanafunzi mara nyingi kwa kipindi cha mwaka mzima.

**Mazoezi binafsi [unatenda]:** Katika hatua hii mwalimu anatakiwa kutoa mazoezi binafsi ya ziada ili kutathmini kama wanafunzi wameweza kusoma kwa haraka na kwa usahihi kwa kuwa husaidia kuelewa kile wanachokisoma.

**Mwalimu**: "kumbuka tunahitaji kusoma kwa haraka na kwa usahihi kwasababu hutusaidia kuelewa kile tulichokisoma. Sasa nitachukua herufi/silabi/neno/sentensi/hadithi na kuisoma kwa haraka bila kukosea na kwa ufahamu. Halafu nataka kila mmoja umsomee mwenzako."



**Kazi ya kufanya: majadiliano katika vikundi**.

Mwezeshaji atawagawa washiriki katika vikundi na kufanya mazoezi mbalimbali ya maandalizi awali, kazi mfano, mazoezi elekezi, na mazoezi binafsi kila mmoja akitoa majibu sahihi kwa mwenzake kisha washiriki watawasilisha kila kazi mbele ya kikundi ambacho nacho kitatoa maoni yake.

## SIKU YA TATU



### Mapitio ya mawasilisho ya siku iliyotangulia (dakika 30)

Mwezeshaji atawauliza washiriki maswali yafuatayo kutoka kwenye mada za siku iliyotangulia
Nini maana ya utambuzi wa umbo sauti (kifonolojia/kifonimu)? mfano
Nini maana ya fonetiki/sauti? Mfano
Nini maana ya ufasaha? Mfano wa kazi za kufundishia ufasaha**.**




**Msamiati (saa 1.30)**

Kama ilivyokuwa awali, mwezeshaji awaambie kuwa kipengele cha nne katika mfuluulizo wa vipengele muhimu vya usomaji ni msamiati. Kipengele hiki ni ufunguo kwa wanafunzi kuelewa kile wanachokisoma. Wanafunzi walio na msamiati finyu watakuwa na wakati mgumu katika kuunda dhana hata kama wanaweza kujifunza kutamka maneno kwa ufasaha.


**Ufafanuzi: ufahamu wa maneno na maana ya neno katika lugha.**
**Umuhimu wa kusoma**
Wanafunzi wanahitaji kufahamu maana ya neno wanalolisoma na hivyo kuweza kukielewa kifungu cha habari.
**Njia mbalimbali za kufundisha maneno mapya.**
Kuwapa wanafunzi njia mbalimbali ili kushughulika na maneno mapya huwasaidia kuongeza uelewa wao kuhusu maneno hayo.
Zifuatazo ni mbinu anuai zilizo rahisi kutumia:

- **Kulinganisha maneno mapya na yale ambayo tayari yanayofahamika**. Hudokeza maneno kwa wanafunzi yanayohusiana na maneno mapya na kuwataka wabaini namna maneno hayo yanavyohusiana.
- **Kutumia maneno mapya katika sentensi**. Ni muhimu kwa wanafunzi kutumia neno jipya katika sentensi inayoonesha kuwa wameelewa maana ya neno hilo.
- **Kuhusisha maana na maneno mapya**. Tumia kazi zinazofanya mazoezi ya aina hii kuwa kiburudisho kwa wanafunzi ikiwa ni pamoja na zile za kucheza. Fafanuzi/maana zilizotolewa na wanafunzi zinaweza kutumika ili kupata maana mbalimbali.
- **Kutumia maneno mapya katika muktadha mbalimbali**. Wanafunzi wanaojifunza maneno na kuyahamishia katika muktadha mwingine wa kimatumizi huonesha kiwango cha uelewa wao kuhusu maneno hayo.

- **Kuwapa wanafunzi mazingira mbalimbali ya utumiaji wa maneno mapya**. Wanafunzi wanahitaji kuona, kusikia, kusoma na kuandika maneno kwa kurudiarudia katika miktadha mbalimbali tofauti ya kujifunza maneno kwa ukamilifu.

Kipengele hiki kina kazi moja inayojirudia rudia. Kazi hiyo iko katika sehemu 3, yaani wanafunzi kurudia rudia neno, kuwauliza wanafunzi kama wanalifahamu neno, kutoa maana kama wanafunzi hawalielewi na kutunga sentensi kwa kulitumia neno hilo.

Wakati mwingine, badala ya kufundisha maneno mapya, walimu watarudia msamiati huo kwa ufupi kwa kuwaongoza wanafunzi watoe maana kwa kila msamiati kutoka siku iliyotangulia na kutoa tathmini rasmi pale inapobidi.
Wakati wa kufundisha msamiati hakikisha sentensi hizo ni kamili kiasi cha kutoa ufafanuzi kuhusu maana ya neno.



**Kazi ya kufanya: majadiliano katika vikundi**
Baada ya kazi mfano ya mwezeshaji, waongoze washiriki kufanya mazoezi katika vikundi kuhusu mbinu za kufundisha msamiati na kubadilishana mawazo kati ya vikundi na vikundi. Kisha ongoza kila kikundi kuonesha matumizi ya mbinu za kufundisha msamiati kwa kikundi kizima na kutoa maoni.




**Ufahamu (saa1.30)**
**Vifaa/zana**: Matini mbalimbali zilizo fupifupi (5-10)
Waambie washiriki kuwa kipengele cha mwisho ni cha ufahamu. Hili ndilo lengo kuu la usomaji. Usomaji haukamiliki mpaka wanafunzi wanapoweza kuelewa kile walichokisoma. Katika kipengele hiki wanafunzi wataweza kusoma ili wajifunze. Kusoma ili kujifunza kutawawezesha wanafunzi kujifunza masomo mengine kama vile Sayansi, Jiografia, Hesabu n.k.

**Maana ya ufahamu:** Ni utaratibu wa kupata maana katika lugha ya mazungumzo na/ au ya maandishi.
**Umuhimu wa kusoma**
- Kupitia ufahamu, dhana/maana hujengwa na wanafunzi huanza kujifunza kwa kusoma.
- Wanafunzi huweza kufundishwa mbinu za ufahamu, njia bora za kufikiri kuhusu matini ili kupata dhana/maana.
- Ufundishaji wa ufahamu huboresha mafanikio ya usomaji na


kuwawezesha wanafunzi kujifunza kutoka katika matini.
- Wanafunzi huweza kujitathmini ufahamu wao.wanahitaji kukuza uwezo wa kuzitambua stadi zao wenyewe.
- Mbinu za ufahamu hutumika kabla wakati na baada ya kusoma,na

Wanafunzi watasoma hadithi moja kila wiki kwa ajili ya kipengele cha ufahamu. Wiki sita za mwanzo zitakuwa kwa ajili ya ufahamu wa kusikiliza ambapo mwalimu husoma hadithi na wiki sita za pili na wiki sita za tatu wanafunzi watasoma hadithi na kufanya kazi za ufahamu wa kusikiliza. Ratiba ya ufahamu kwa kila wiki itakuwa katika mfumo ufuatao:

**Siku ya kwanza**
- Kufundisha msamiati/maneno mapya.
- Wanafunzi hutumia kichwa cha habari au picha kubashiri hadithi inahusu nini.
- Kusoma hadithi na kutafuta kama utabiri wao ulikuwa sahihi.

**Siku ya pili hadi ya tatu**
- Marudio ya msamiati.
- Kusoma hadithi.
- Kufundisha mbinu za ufahamu.

**Siku ya nne**
- Marudio ya msamiati.
- Kusoma hadithi.
- Kujibu maswali yanayojitokeza.



**Kazi ya kufanya kwa vikundi: Majadiliano katika vikundi**
Mwezeshaji atawasilisha mbele ya kikundi kizima hadithi fupi fupi tatu kutoka kitini cha kufundishia cha mwalimu. Baada ya kila kazi, vikundi vitapewa fursa ya kufanya mazoezi ya kazi iliyowasilishwa. Mara baada ya hadithi zote kuwa zimewasilishwa na kufanyiwa mazoezi watu watatu kutoka kwenye kikundi watawasilisha kila kazi mbele ya wenzao.

**Muundo wa matini.**
Matini zilizo nyingi hasa za hadithi zina mtiririko wa matukio. Kuelewa msuko wa matukio kutawasaidia wanafunzi kuielewa hadithi. Aidha, kuielewa mbinu hii kutawasaidia wanafunzi wanaposoma matini zenye taarifa zaidi zinazofundisha jinsi ya kufanya jambo hatua kwa hatua. Pia hii ni hatua ya kwanza katika kujifunza kufupisha hadithi au matini.

Kwa kutumia mbinu hii mwalimu atawafundisha wanafunzi kuwatambua wahusika wakuu, muundo, na tukio kuu kwa kuuliza nini kilitokea kwanza, kipi kilifuata na kipi kitatokea mwisho.

**Muundo wa hadithi**
Kwa ujumla hadithi huundwa na wahusika wakuu, muundo, mgogoro na suluhisho. Kufahamu jinsi ya kuvipata vipengele hivi katika hadithi itawasaidia wanafunzi kuielewa hadithi kwa urahisi zaidi.


<u>Mhusika mkuu</u>: mtu/ kitu muhimu ambacho hadithi au kisa kimejengwa juu yake.
<u>Mandhari</u>: Mahali na wakati kisa kilipotendeka.
<u>Mgogoro</u>: Mgongano wa wahusika katika hadithi.
<u>Suluhisho</u>: Tukio/ njia iliyotumika kutatua mgogoro.

**Utaratibu wa kufundisha: Jinsi ya kufundisha ufahamu.**

**Maandalizi awali: kuwaeleza wanafunzi watakachojifunza na umuhimu wake.**

**Mwalimu: "**Tutasoma mengi kuhusu Rehema na Sokwe mzee kutoka katika kitabu chetu, ili kuelewa kile mnachokisoma nitawafundisha mbinu rahisi ya kuelewa na kukumbuka hadithi. Katika kufanikisha hili nitawasaidieni mbinu sahihi za kuwatambua wahusika wakuu, mandhari, migogoro na suluhisho kama ilivyojitokeza katika hadithi"

**Kazi mfano[ninatenda]:** Toa maelezo bainifu ikiwa ni pamoja na kuonesha mbinu**.**
**Mwalimu:** kwa kuanza, anza na mfano, "nitasoma hadithi kisha nitatumia wahusika wakuu, mandhari, mgogoro na suluhisho ili kuielewa hadithi."
**Mazoezi elekezi[tunatenda]:** mwalimu huhamisha taratibu jukumu la kuielewa hadithi kwa kuwahamasisha wanafunzi kuibua wahusika wakuu, mandhari, mgogoro na suluhisho kutoka kwenye hadithi na mwisho kuwaruhusu kufanya kazi katika jozi ili kueleza upya maudhui ya hadithi.
**Mazoezi binafsi [unatenda]:** Baada ya wanafunzi kuwa na fursa ya kubainisha wahusika wakuu, mandhari, tatizo na suluhisho wakilenga kwenye maudhui ya hadithi, waongoze kila kikundi kuelezea upya jinsi walivyoielewa hadithi.



**Kazi ya kufanya kwenye vikundi: majadiliano**


Mwezeshaji awaongoze washiriki kufanya kazi katika vikundi ili kubainisha wahusika wakuu, mandhari, migogoro, na suluhisho wakihusisha na hadithi iliyotolewa kwa kila kikundi. Baada ya hapo,kila kikundi kitawasilisha kile walichokielewa kutoka kwenye hadithi.

## Maelezo ya jumla kuhusu mpango wa kusoma

Mpango wa kusoma umejikita katika mawanda na mtiririko mahsusi katika kujifunza kusoma Kiswahili. Mpango huu uliandikwa na wataalamu kutoka Taasisi ya Elimu Zanzibar,Taasisi ya Elimu Tanzania, wataalamu kutoka Vyuo vya walimu, Wakaguzi wa shule, na walimu.

**Mawanda** ni dhana/maudhui yatakayofundishwa kwa walengwa mahsusi na **mtiririko** ni mpangilio ambamo maudhui hayo yatafundishwa. Kwa mpango huu, mawanda ni sauti za herufi na stadi za kusoma huku mtiririko ni mpangilio ambamo stadi hizo zitafundishwa.

Ndani ya mpango huu, herufi mpya mbili zitafundishwa kila wiki, herufi tatu zilizotangulia zitakuwa zinarudiwa kila siku, Ijumaa yatakuwa ni marudio ya wiki na wiki ya nne itakuwa ni marudio ya mwezi mzima.



**Kazi ya kufanya katika vikundi: Majadiliano**

Fungua masomo ya wiki ya tano za mwanzo kwenye muongozo wa somo kisha pitia masomo hayo na kubainisha kile kilichofundishwa na kilifundishwa kwa mpangilio gani. Unagundua nini kuhusu vitamkwa vilivyokuwa vikifundishwa?

"*Kwa kuwa tunahitaji wanafunzi kuwa na uwezo wa kusoma hata maneno machache kwa haraka iwezekanavyo, tutafundisha herufi katika mpangilio unaojikita katika ufasaha na uwezo wa kuunda maneno madogo madogo ya kawaida. Katika wiki chache za mwanzo wanafunzi watajifunza irabu na konsonanti pamoja na marudio ya sauti ya sauti zilizofundishwa mwanzoni. Kisha watаunda maneno kwa kutumia vitamkwa/ sauti walizokwishajifunza, aidha stadi zitafundishwa kwa mpangilio wa kutoka rahisi kwenda magumu kwa kila kipengele cha kusoma*"

## Vipengele vya kila somo

Angalia katika andalio la somo(muongozo wa mwalimu), kisha bainisha vitu vinavyounda somo zima. Utagundua kuwa katika muongozo huu vipengele vifuatavyo vimezingatiwa, fonimu, sauti, ufasaha, msamiati na ufahamu ambavyo vitafundishwa kila siku.

**Daftari la mazoezi ya mwanafunzi**

Katika kila somo la wiki herufi tatu za masomo yaliyotangulia zitakuwa zinarudiwa na herufi moja mpya itakuwa inafundishwa.


Herufi itafundishwa kwa kuanza na herufi ndogo kisha herufi kubwa. Sehemu tatu zilizobaki ni za silabi, maneno na sentensi. Kila sehemu itakuwa na marudio na mambo mapya. Maudhui mapya yamewekwa katika herufi zilizokolezwa.



**Umuhimu wa kujifunza sauti (Saa 1)**

Mwezeshaji asisitize kuwa kujifunza kusoma ni kujifunza sauti za lugha. Ni muhimu kwa wanafunzi kujifunza sauti kwa usahihi. Ili kufanikisha hili, ni muhimu kwa walimu kuzisikiliza na kuzitamka sauti kwa usahihi ili waweze kuwa mfano na kutoa majibu yanayostahili kwa wanafunzi.

Kila herufi inatakiwa kutamkwa kwa sauti moja tu unapoonesha jinsi ya utamkaji wa sauti /b/ na siyo /ba/. Ni muhimu kwa mwalimu kuepuka kuongeza irabu kwenye konsonanti zinapotamkwa kwa lengo la kuwaelekeza wanafunzi.



**Kazi ya kufanya: Tamka neno kisha uliza ni neno gani**

Mwezeshaji atatumia kadi za herufi, anaonesha kila herufi na kuzitamka kwa usahihi huku washiriki wakifuatisha anavyotamka. Mwezeshaji atatumia karatasi za mazoezi zenye herufi zinazofananishwa na picha kuwasaidia washiriki kuzikumbuka sauti.



**Utaratibu wa kufundisha: Jinsi ya kufundisha stadi mpya (dakika 45)**

Mwezeshaji asisitize vipengele ambavyo vinajirudia katika muongozo wa wa mwalimu wa kufundisha usomaji kwa darasa la kwanza na la pili. Kila kazi inafuata mfumo unaojirudiarudia kama vile maandalizi awali, kazi mfano, mazoezi elekezi, na mazoezi binafsi. Sasa tupitie kila kimoja kwa ufupi.

**Maandalizi awali**

Hii ni zana inayomsaidia mwalimu kuwaelekeza wanafunzi kuyafikia mazoezi mapya au maelekezo kuhusu kazi zilizoandaliwa kwa ajili yao.

Wanafunzi wanapoelewa kile wanachokifanya na jinsi ya kukifanya, wanafanya kazi kwa kwa uhuru zaidi na kupata maendeleo makubwa kitaaluma.

Unapofundisha dhana mpya kwa wanafunzi itawachukua muda kuilewa, lakini wanapokuwa wameifanya kwa siku chache unatakiwa kuongeza kasi.

Utatumia muda mwingi mwanzoni mwa mwaka na muda kidogo kadri unavyosonga mbele.

**Mfano:**
**Mwalimu**: "Sasa tutajifunza kutamka herufi ***n***. Tutatumia sauti ya herufi hiyo kusoma na kutamka maneno"

**Kazi mfano[ninatenda]:**
Wakati wa kazi mfano kila stadi inafafanuliwa vizuri na kuondoa kila hali ya utata katika kazi ya ufundishaji na ujifunzaji.

Kuondoahaliyautatakunatuhakishiakuwawanafunzihawatachanganyikiwa wala kupotea kwa kuwa hali hiyo ikitokea wanafunzi hawawezi kujifunza. Katika kulifanikisha hili, mwalimu anapaswa kuweka wazi lengo na kutoa muongozo wa wazi unafuata hatua hatua katika kujifunza dhana iliyokusudiwa.

**Mfano**: Mwalimu huonesha herufi ubaoni (kwa kutumia zana) na kusema,
**Mwalimu**: sauti ya herufi **n** ni /nnn/

**Mazoezi elekezi[tunatenda]:**
Kama tulivyojifunza katika mawasilisho yaliyotangulia, mazoezi elekezi huwawezesha wanafunzi kufanyia mazoezi kile walichoona mwalimu akifanya. Mwalimu amefundisha stadi mpya, na wanafunzi watafanya mazoezi pamoja wakiongozwa na mwalimu.

**Mfano**. "Sasa tufanye kwa pamoja. Sauti ya herufi **n** ni /nnn/."
**Mwalimu na wanafunzi**: wanatamka sauti /nnn/.
**Mazoezi binafsi [unatenda]**
Mara baada ya darasa zima kuwa limefanya mazoezi, mwalimu anatakiwa atoe nafasi kwa vikundi vidogo vidogo na wanafunzi mmoja mmoja kuonesha kile walichojifunza kwa kuwataka wafanye mazoezi peke yao. Hii itamsaidia mwalimu kupata idadi ya wanafunzi walioelewa, pia humsaidia pia katika kutoa maamuzi kuhusu kuendelea kufanya mazoezi au kusonga mbele.
Mazoezi haya huwapa wanafunzi fursa ya kufanyia mazoezi ya kile walichojifunza. Baadhi ya wanafunzi huhitaji mazoezi kidogo na wengine mazoezi mengi. Wanafunzi wasishiriki katika mazoezi haya kabla ya kulimudu somo peke yao.

Mfano. Sasa mnafanya peke yenu. Sauti ya herufi n ni ___

Ndugu mshiriki zipo njia anuai anazoweza kuzitumia mwalimu katika mazoezi binafsi. Anatakiwa kuzitumia kadri awezavyo ili wanafunzi wawe tayari wakati wote kumwelewa na kuhakikisha kuwa anakipata kile walichojifunza wanafunzi. Mwalimu anatakiwa kuwafikia wanafunzi wote darasani mmoja mmoja na katika vikundi vidogo vidogo kama ifuatavyo:

Mfano - Mwalimu: wavulana, sauti ya herufi hii ni ___


Mfano - Mwalimu: wasichana, sauti ya herufi hii ni ___

Mfano - Mwalimu: wanafunzi walio mistari miwili ya mwisho, sauti ya herufi hii ni ___

Mfano - Mwalimu: wanafunzi walio kulia mwa darasa, sauti ya herufi hii ni ___

Mfano - Mwalimu: wanafunzi walio nyuma, sauti ya herufi hii ni ___

Mfano - Mwalimu: wanafunzi ambao majina yao huanza na herufi (mfano. n) ___



**Kazi ya kufanya: Mazoezi**

Mwezeshaji awaongoze washiriki hatua zote za ufundishaji wa herufi ***m***. Katika kila kikundi mtu mmoja atakuwa mwalimu na wengine watakuwa wanafunzi kwa kutumia utaratibu wa kufundisha kama ulivyooneshwa hapa chini

**Maandalizi awali**
“Leo tutabainisha na kutamka kitamkwa cha mwanzo katika neno. Kwanza nitatamka neno, nanyi mtafikiria kuhusu kitamkwa cha mwanzo na nitakaposema “kitamkwa cha mwanzo”, mtanitajia kitamkwa cha mwanzo cha neno hilo”.
**Kazi mfano: Taja neno inayokusudiwa.**
Mwalimu: Neno ni _pata__ . Bainisha kitamkwa cha mwanzo kisha kitamke.
Mwalimu: Neno ni___pata___. Kitamkwa cha mwanzo ni _/p/___ hivyo natamka / p /
**Mazoezi elekezi**
Mwalimu: twende pamoja. Neno ni _pata___. Kitamkwa cha mwanzo ni __p__ hivyo natamka /p /
Mwalimu na wanafunzi wanatamka kitamkwa cha mwanzo cha neno.
Endelea na mifano miwili mpaka mitatu.
**Mazoezi binafsi**
Mwalimu: sasa nitatamka neno na mtataja kitamkwa cha mwanzo cha neno hilo.
Mwalimu: Kitamkwa cha mwanzo katika neno **kaka** ni _____. Wanafunzi wanajibu /k/




**Tathmini (saa 1)**
Tathmini ni sehemu muhimu katika la kufundisha na kujifunza. Ili kuelewa kama wanafunzi wamefahamu kile walichofundishwa, lazima walimu wafanye tathmini ya somo husika.. Pia hii itamsaidia mwalimu kufahamu kuwa wanafunzi wamepata maarifa yaliyokusudiwa. Aidha, itawasaidia kufanya maamuzi juu ya kuendelea na mada mpya au kurudia somo au kutoa mazoezi zaidi. Katika programu hii, walimu watatathmini ufahamu wa wanafunzi kwa njia tatu tofauti:

- Mazoezi binafsi kila mwisho wa somo.
- Upimaji wa kila wiki ambao hufanyika siku ya tano.
- Upimaji wa maendeleo ya kila mwezi ambao hufanyika kila wiki ya nne.

**Mazoezi binafsi**
Wambie washiriki kuwa, sehemu hii inapaswa kuwasaidia walimu kufahamu kama wanafunzi wameelewa kile kilichofundishwa kwa wakati huo.
Kugundua mapema matatizo ya kutokuelewa au kuelewa visivyo ni njia bora zaidi ya kuhakikisha kuwa wanafunzi wamejifunza stadi fulani na kuwa hali inaruhusu kusonga mbele.

**Tathmini ya kipindi cha siku ya tano**

Ndugu mshiriki, tathmini hii itafanyika kila Ijumaa au siku ya tano ya ufundishaji. Somo litahusu kutathmini herufi, silabi, maneno na sentensi zilizofundishwa kwa kipindi hicho.

Tathmini hii iko katika andalio la somo na itakuwa ni fursa muhimu kwa walimu kufahamu kama wanafunzi wamejifunza yote wanayohitaji kufahamu au kama maudhui fulani yanahitaji kufundishwa tena au kutoa mazoezi zaidi.

**Upimaji wa maendeleo kwa kipindi cha wiki ya nne**

Wiki moja mwishoni mwa kila mwezi itakuwa kwa ajili ya upimaji wa maendeleo yaliyofikiwa. Lengo la upimaji huu ni kupata kiwango cha kila mwanafunzi alichofikia, wanachokifahamu na wasichokifahamu na maendeleo yao kulingana na malengo ya kusoma kwa ufasaha na ufahamu. Wiki hii itakuwa katika sehemu tatu:

Marudio: kwa kushirikiana na walimu, wanafunzi watafanya marudio kuhusu ufahamu wa herufi, silabi maneno na sentensi kwa siku moja hadi mbili..


**Tathmini:** mwalimu atamtahini kila mwanafunzi katika ufahamu wa herufi, silabi na maneno na kutaka wasome na kujibu maswali ya ufahamu. Hili litachukua siku mbili hadi tatu kulingana na idadi ya wanafunzi waliomo darasani. Mwalimu atapitia taarifa alizokusanya kutoka kwenye tathmini na kuzitumia kuamua kipi kinahitaji kurudiwa kufundishwa au kufanyiwa mazoezi tena.

Kurudia kufundisha: mwalimu atatumia siku moja hadi mbili kufundisha tena na kutoa fursa ya kufanya mazoezi pale yanapohitajika.

## Kufahamu muongozo wa mwalimu

Ni muhimu kwa mshiriki kujua kuwa katika programu hii kipengele muhimu ni utaratibu wa kufundisha usomaji katika madarasa ya awali ambao unatumika sanjari na muongozo wa mwalimu.


Muongozo huu unatumia mfumo duara katika ufundishaji na unafundisha kila somo kwa mifano na kutathmini maendeleo ya mwanafunzi. Ni muhimu kwa walimu kufuata kwa makini muongozo uliotolewa ili kuwawezesha wanafunzi kunufaika na mpango huu.



**Kazi ya kufanya: Kibanda cha Scavenger na vitini vya mwalimu**

Washiriki wagawanyike katika vikundi vya watu watano hadi kumi na kufanya kazi kwa pamoja kuangalia masomo yaliyoandaliwa na kitini cha mwalimu cha kufundishia ili kupata vitu viliyomo kwenye orodha. Kila kikundi kinatakiwa kufafanua kila kipengele kwa kutoa mifano miwili.

- Utaratibu wa kufundisha
- Lengo
- Utambuzi wa fonimu
- Sauti
- Marudio kuhusu ufasaha
- Ufahamu
- Maandalizi awali
- Kazi mfano
- Mazoezi elekezi
- Mazoezi binafsi



**Kazi ya kufanya kwa kila mshiriki: Majadiliano ya kuhitimisha mafunzo**

Washiriki wajadili katika jozi kisha katika kikundi maswali yafuatayo:

- Kipi kilikuwa cha manufaa/thamani sana kuhusu mafunzo haya?
- Ni changamoto zipi zilizojitokeza katika mafunzo haya?
- Kwa kiasi gani mafunzo yamekidhi matarajio yako?
- Nini kifanyike ili kuimarisha mafunzo yajayo?
- Ni mabadiliko yapi yanaweza kujitokeza katika shule yako kutokana na mafunzo haya?

# Marejeleo


Institute of Kiswahili Research (2006). English – Swahili Dictionary 3rd Edition; Mauritius, MSM Ltd.

IRA (2006). Mbinu Bainifu Kwa ajili ya Kufundisha Elimu ya Msingi . Muongozo wa Mwezeshaji: Dar es salaam

Kiswahili Kitabu cha pili, Mwanafunzi – Zanzibar.

Kiswahili Kitabu cha Kwanza, Mwanafunzi – Zanzibar.

Malawi Teacher Professional Development Support; Reading Intervention Program (USAID/MALAWI).

Oxford University Press (June 2012). Kiswahili Shule za Msingi Chapa ya saba.

Pili, Dumea et al (2011). Muongozo wa Ufundishaji na Ujifunzaji katika Madarsa ya Shule za Msingi: Mradi wa Vitabu vya Watoto.

Sylivia Linan – Thompson et al (2007). Research – Based Methods of Reading Instruction for English Language Learners; Printed in USA.

WEU (2004). Mafunzo ya Ualimu Kazini. Muongozo wa Kufundisha Kwa Kutumia Njia/Mbinu Shirikishi: Romeja’s Limited , Dar es salaam.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi (2005 ). Muhtasari wa Kiswahili Kwa Shule za Msingi, Taasisi ya Elimu Tanzania.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi (2010). Moduli ya Ujuzi wa Kufundisha kwa Umahiri.